Nipashe
Jumapili Agosti 1, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
JUMAPILI
ISSN 0856 • No. 0580659




UKURASA 15

**MAFUTA YA MAWESE** Furahia ngozi laini inayoita

UKURASA 14



**ASKOFU** aona shida elimu chanjo corona maeneo ya vijijini

UKURASA 3

# Kilichojificha hasara ATCL



Uongozi wa shirika waorodhesha vikwazo, Rais Samia akiri... *UK. 4*



## POLISI MBARONI KWA TUHUMA KUTOROSHA MADINI DHAHABU

UKURASA 5

## YALIYOMO

UKURASA WA 8

### NAMNA KUEPUKA WAKWE, NDUGU KUINGILIA NDOA

MOJA ya mambo ambayo husababisha ndoa kuvurugika na hata kuvunjika ni wakwe na ndugu kuingilia kati. Lakini kuna mambo kadhaa ya kuzingatia ili kuepuka hali hiyo. Ni mambo gani hayo? ....

# Viuatilifu feki vyanaswa, wafanyabiashara kukiona

UK. 2

**MICHEZO** YANGA, BULLETS MAJARIBUNI LEO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Viuatilifu feki vyanaswa

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, ameagiza maduka yaliyohusika na kuwauzia wakulima wa mkoa huo viuatilifu vilivyoisha muda wake, yafungiwe kwa muda wakati taratibu za kisheria zikiwa zinaendelea dhidi ya wamiliki wake.

Amesema lengo la kufunga kwa muda maduka hayo ni kuzuia kuendelea kusambazwa pembejeo hizo alizotaja zinarudisha nyuma jitihada za wakulima katika kujikwamua kimaisha.

Brigedia Jenerali Gaguti alitoa agizo hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari na kuelezea mafanikio ya msako wa siku mbili uliokamata tani 84.3 za viuatilifu vya Salfa vilivyoisha muda wake pamoja vipande 292 vya viuatilifu maji. Alisema kuwa katika msako huo, watu 15 wanaodaiwa kuhusika na usambazaji na uuzaji wa viuatilifu hivyo, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa ajili kukamilisha taratibu za kuwafikisha mahakamani.

"Tulipata taarifa ya kuwepo kwa viuatilifu vilivyoisha muda wake ambavyo wakulima wetu wanauziwa, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vikafanya operesheni iliyowakamata watu 15 pamoja na hizo tani nilizozitaja.

"Hawa wanatumia nafasi hii ya uhitaji wa wananchi kuhudumia mashamba yao na wao wanawauzia dawa zilizoisha muda wake," alisema Brigedia Jenerali Gaguti.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mtwara kuwa makini na dawa wanazonunua kwa ajili ya kuhudumia mikorosho yao, huku akisisitiza serikali itaendelea kuwasaka na kuwakamata watu wote wanaotaka kuhujumu jitihada za wakulima katika kujipatia mazao bora.

Kiongozi huyo alisema zao la korosho linachangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa na lisipopata viuatilifu sahihi, litakufa na nchi itakosa mapato kupitia zao hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Marc Njera, alisema uchunguzi wa awali umeonyesha viuatilifu vilivyokamatwa vilifutwa tarehe ya kuonyesha mwisho wa matumizi yake.

Alibainisha kuwa mbali na kufutwa tarehe ya mwisho wa matumizi, wahusika pia wanatuhumiwa kughushi barua za taasisi ya udhibiti wa viuatilifu (TPRI), ikionyesha wameruhusiwa kuuza dawa hizo baada ya muda wake wa matumizi kumalizika.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Vijana Tayoa, Peter Masika (kushoto), akifafanua jambo kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, kuhusu makasha yanayotumika kusambazia kondomu, wakati wa uzinduzi wa makasha hayo, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yaona uhaba wataalamu wa madini

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, amevitaka vyuo vikuu kuweka mkakati wa uzalishaji wa watalaamu wa kutosha hususan Sekta ya Madini ili kufikia lengo la taifa la kuwa nao 98,000 ifikapo mwaka 2025/26.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifunga Maonyesho ya 16 ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).

Alisema vyuo vikuu na taasisi za utafiti hazina budi kujikita katika utafiti na uvumbuzi wa matatizo mbalimbali ya kijamii na kiuchumi.

Alisema ukuaji wa uchuni unategemea uwapo wa rasilimali watu wenye ujuzi wa ubunifu wa mambo mbalimbali.

Alisema takwimu za mwaka 2016 zinaonyesha wataalamu wenye ujuzi wa hali ya juu ni asilimia 3.3 na wenye ujuzi wa kati ni asilimia 17.

Alisema bado taasisi za elimu ya juu zina kazi za kuongea asilimia hizo.

Alitaja mafanikio ya Sekta ya Elimu tangu 2015 kuwa ni pamoja na kuongeza wadahiliwa, wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu na kuboresha miundombinu ya kujifunzia.

Alisema ili kujenga uchumi shindani, hawana budi kuwekeza katika utafiti na ubunifu na serikali imedhamiria kuwekeza katika hilo.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alisema kwa muda wa siku sita tangu kufunguliwa kwa maonyesho hayo, wanafunzi wa shahada 52,336 wametuma maombi yao katika taasisi mbalimbali za elimu ya juu zilizoshiriki.

Alisema maonyesho hayo yamekutanisha jumla za taasisi za elimu ya juu 74.

Alisema wataendelea kushirikiana na taasisi hizo ili ziendelee kutoa elimu bora kwa kuzijengea uwezo.

Akizungumza kwa niaba ya taasisi za elimu ya juu zilizoshiriki maonyesho hayo, Dk. Ali Makame Ussi kutoka Chuo cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) alisema mkusanyiko huo ni muhimu kwa sababu unatoa nafasi kwao kukutana na kubadilisha uzoefu wa shughuli wanazofanya.

Pia alisema wanapata fursa ya kujifunza na kupata mawazo mapya ili kuja na ubunifu zaidi na kuwawezesha vijana kufanya uchaguzi sahihi wa vyuo wanavyotaka kwenda kusoma.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya TCU, Charles Mgone, alisema wameshuhudia mageuzi mengi ndani ya tume.

# Waitara apongeza utendaji wa TBA

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, amekutana na menejimenti ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na kusifu utendaji wao wa kazi.

Kikao hicho kilifanyika juzi mkoani Dar es Salaam baada ya kiongozi huyo kutembelea mradi wa nyumba za Magomeni Kota na kubainisha kufurahishwa na namna ambavyo TBA wameonyesha ubunifu mkubwa katika ujenzi wa nyumba hizo hasa kwa kutumia wataalamu wa ndani.

Alisema TBA wanastahili pongezi kwa kujenga majengo yenye ubora na viwango vya juu ambayo yapo katika mfumo wa kisasa.

"Ninaipongeza TBA kwa kujenga majengo ya kisasa, lakini pia kwa kujenga majengo yenye viwango vikubwa kwa kutumia wataalamu wa ndani.

"Hapa ngoja nilitolee mfano jengo la Simeoni Arusha ambalo nililitembelea hivi karibuni. Kama lile jengo likikamilika, litatatua changamoto kwa kiasi kikubwa ya makazi kwa watumishi wa umma.

"Lipo katika mfumo wa kisasa. Kwa hiyo TBA wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana," Waitara alisifu.

Naibu waziri huyo pia alitoa pongezi kwa TBA kwa kazi nzuri katika mradi wa nyumba za Magomeni Kota.

"Niwapongeze pia TBA katika mradi wa Magomeni Kota, ukiangalia huu mradi utagundua kuna ujenzi wa ziada umeongezwa na umeongeza tija na ufanisi katika mradi huu.

"Utaona wamebuni ujenzi wa ziada wa vizimba kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga pamoja na kuweka maduka ya kisasa yatakayosaidia katika utoaji wa huduma kwa wakazi wa watakaoishi humu ndani," alipongeza.

Waitara pia aliitaka TBA kusisitiza usimamizi mzuri katika miradi hiyo ikiwamo kutoa elimu kwa watakaokuwa wakazi wa nyumba hizo na namna bora ya utunzaji wa mazingira na miundombinu hiyo.

Mtendaji Mkuu wa TBA, Daudi Kondoro, alimshukuru naibu waziri kwa kutembelea miradi mbalimbali ya TBA na kumthibitishia kuyafanyia kazi maelekezo yote aliyoyatoa.

# HABARI KITAIFA

## Mtaalamu: Sheria ya madeni imulikwe

**Na Beatrice Moses**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi Isiyokuwa ya Kiserikali Inayofuatilia Madeni na Maendeleo Tanzania (TCDD), ameishauri serikali kuangalia upya sheria inayohusu madeni ya nchi ili kuleta nidhamu na uwajibikaji katika matumizi ya fedha.

Hebron Mwakagenda amesema hatua hiyo inapaswa kwenda sambamba na kuunda mfumo mpya utakaoshirikisha Bunge katika mchakato wa ukopaji na urejeshaji wa madeni.

Mkurugenzi huyo alitoa rai hiyo jana alipofungua mkutano uliolenga kutoa elimu kuhusu Deni la Taifa.

Alisema ni vyema ukopaji na urejeshaji wa madeni uwekwe kwenye mfumo mzuri ili kulipunguzia taifa mzigo wa madeni ambao unaweza kuleta athari ya nchi kudidimia kiuchumi pamoja na kushindwa kutoa huduma muhimu kwa jamii.

"Ifike wakati kukawekwa mifumo ya ukopaji kwa kulishirikisha Bunge, hii itapunguza ukopaji usio na tija ambao hata Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG0 imekuwa ikibaini kasoro kadhaa katika ukopaji na matumizi ya fedha hizo za mikopo," alisema.

Mwakagenda aliongeza kuwa ni muhimu kukopa kwa tija na fedha hizo zitumike kwa faida ya jamii ya sasa na kizazi kijacho.

Alisema kwa sasa mfumo wa ukopaji umebadilika kwa kuwa badala ya kukopeshana nchi kwa nchi, imehamia kwenye biashara, hivyo kusipowekwa umakini, taifa litadidimia kiuchumi kwa sababu ya kuelemewa na madeni.

Alisema asilimia 60 ya fedha za serikali zipo kwenye ununuzi, hivyo ni muhimu zisimamiwe vyema ili zilete matunda katika utoaji huduma.

Alisema TCDD kwa kushirikiana na nchi nne za Afrika Mashariki, wamefanya utafiti kuhusu madeni kwenye nchi husika kwa lengo la kujenga uelewa na umuhimu wa uwazi katika nchi hizo. Mchungaji wa Kanisa la Kisabato Tanzania, Elisante Jackson, alisema serikali inapaswa kuwa wazi wakati inaingiia mikataba mbalimbali ili kuondoa sintofahamu kwa jamii kuhusu madeni.

Alisema katika kuhakikisha serikali inajenga uhusiano mzuri na wananchi wake, ihakikishe inaondoa sheria kandamizi.

Pia aliomba serikali izingatie Sheria ya Ununuzi kwa kuwa itasaidia kuondoa kasoro zinazojitokeza kwenye baadhi ya maeneo ya kiutendaji hivi sasa.

Jackson alisema ili kupata kodi za kutosha, ni vyema serikali ikajenga uhusiano mzuri na wafanyabishara kwa kuwa itasaidia kuzuia mianya ya ukwepaji kodi.

"Upo umuhimu wa viongozi wa dini katika masuala mbalimbali ya kitaifa, wakishirikishwa ipasavyo katika michakato, itasaidia kuinua uchumi wa nchi," alisema Jackson.

Aliwataka viongozi wa kisiasa kukubali kukosolewa kwa kuwa matamko yao wanayoyatoa mara nyingi hayana afya kwa jamii.

Mjumbe wa Bodi ya TCDD, Camilius Kassala, kutoka Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), alisema viongozi wa dini wana fursa ya kupaza sauti kwa jamii na hata kwenye masuala ya madeni na maendeleo ili kutoa maarifa, elimu na hekima.

"Viongozi wa dini kwa pamoja wakishiriki kupaza sauti na kutoa elimu kuhusu ukopaji wenye tija, itasaidia kujenga nidhamu kwenye natumizi ya fedha,' alisema Kassala.



Vijana wahitimu wa mafunzo ya programu ya miezi sita ya 2jiajiri, inayofadhiliwa na Benki ya KCB Tanzania, wakionyesha vyeti vyao baada ya kukabidhiwa katika semina ya mafunzo elekezi ya siku tatu, jijini Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Askofu ataka elimu chanjo corona vijijini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Central Tanganyika (DCT), Dk. Dickson Chilongani, ameishauri serikali kutoa elimu ya kina kwa wananchi juu ya upatikanaji wa chanjo ya UVIKO- 19, ili kuondoa dhana iliyojengeka kwa jamii ya pembezoni kuwa wakichanjwa itasababisha damu kuganda na vifo.

Askofu Chilongani aliyasema hayo juzi katika mkutano wa DCT wa Sinoni ya 21 uliofanyika jijini Dodoma, ukifanyika sambamba na uchaguzi wa Katibu wa Sinoni.

Dk. Chilongani alisema kila wanapokwenda vijijini na sehemu nyingine kutoa kipaimara kwa watoto, wanapoihubiria jamii kuhusu kupata chanjo, wengi wao wanasema hawezi kuchanjwa kwa sababu wanachojua chanjo hizo zina madhara na mtu akichoma, damu inaganda na kusababisha kifo.

Alisema jamii inasema hivyo kwa sababu wanasiasa tokea awali wamewajengea wananchi imani kwamba chanjo ni mpango wa wazungu kutaka kuwaua Waafrika, hivyo nao hawachanjwi. "Ni vema serikali kuchukua jukumu la kuwapa wananchi elimu ya kutambua umuhimu wa chanjo kwa sababu viongozi wa dini tunapata shida kuwaelewesha lakini hawaelewi.

"Na hii inatokana na wanasiasa walivyowajengea toka mwanzo kuwa chanjo ni mpango wa wazungu," alisema Dk. Chilongani.

Alisema inabidi serikali ichukue hatua ya kutoa elimu kwa wananchi kupitia wataalamu wa afya ili jamii ijue na kuamini chanjo hizo ni kinga bora kwa afya zao kwa ajili ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Mbali na hilo, askofu huyo alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na kuongoza upataji chanjo, hivyo akasisitiza serikali itoe elimu kwa jamii husani wanaoishi pembezoni ili waweze kupata chanjo.

Alisema kuhusu suala zima la maendeleo ya elimu kuanzia ngazi ya msingi sekondari na vyuo vya DCT, Dayosisi imetoa mapendekezo ambayo yatafanyiwa kazi ili ufaulu uzidi kuongezeka na kufika kiwago cha juu zaidi ya ilivyo sasa.

Askofu Chilongani pia alisisitiza suala zima la watumishi wa DCT hususani wachungaji, maaskofu na wengine wanapotumikia kanisa, wasisahau familia kwa sababu mwisho wa siku wanakwenda kustaafu na kuachia madaraka.

"Nisingependa kuona watumishi wa Mungu wanastaafu halafu anakuwa hana mahali pa kuishi, tunapaswa tuangalie pande zote mbili, kanisa na familia kwa ujumla ili kuepusha malumbano pale unapostaafu kazi ya utume wa Mungu," alitoa angalizo.

Askofu Yona Muhegwa wa Kanisa la Anglikani Parishi ya Msangalale, alisema elimu kwa jamii inahitajika kwa kiasi kikubwa ili ipate chanjo ambazo zitasaidia kujikinga na baa hilo.

## 'Vijana tuchanje kuikabili corona'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UONGOZI wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), umewataka vijana nchini kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Katibu Mkuu wa umoja huo, Kenani Kihongosi, alitoa rai hiyo jana alipozindua Vijana Jogging Club Dodoma.

Kihongosi alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuleta chanjo nchini, akiwataka vijana kwenda kuchanja na kuachana na wanaobeza na kupinga.

Alisema kuwa wengi wa wanaopinga chanjo hiyo, hawajafikiwa na baa hilo au kuondokewa na ndugu zao.

Alisema chanjo hiyo ni ya hiari, hivyo vijana wenye fursa waende wakachanje ili kulinda afya zao dhidi ya maambukizi hayo.

"Akili za kuambiwa changanya na za kwako, nendeni mkachanje kama mlivyoona Rais amezindua utoaji chanjo, hawezi kuingiza nchi kwenye mambo yasiyofaa," alisema.

Kiongozi huyo alisema kila mtu ni shahidi wa vifo vinavyotokea kutokana na ugonjwa huo, hivyo ni muhimu kwenda kupata chanjo.

"Tangu wakiwa watoto wamechanja chanjo nyingi na wengine wamekunywa hata kikombe cha babu, hivyo serikali imesema chanjo hiyo ni hiari, lakini vijana watumie fursa hiyo kwenda kuchanja ili wakinge familia zao,"alisema.

Pamoja na hayo, aliwataka vijana nchini kuilinda amani na kusimamia nchi.

Aliwataka wenyeviti na makatibu wa umoja huo kwenye mikoa na wilaya kuanzisha vikundi vya jogging ili kuimarisha afya zao na kujilinda na maambukizi ya magonjwa mbalimbali ikiwamo corona.

Awali, Mbunge wa Dodoma, Anthony Mavunde (CCM), alimpongeza katibu huyo kwa kushirikiana na vijana kufanya mazoezi ambayo yamekuwa yakihamasishwa na Rais Samia.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**BORNIVENTURA THOMAS** PIUS anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI aina ya **TOYOTA MARK X** yenye namba za usajili T 147 DRS. Chasis No. **GRX1200065473,** Engine No. **4GR0190513** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOM/RB/377641/2021.**

116387802



**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**SHAURI LA MIRATHI NA. 03/2019**

**RUTH JOHN MAKUNE..........................................MDAI**

**DHIDI YA**

**JOHANA MAKUNE SHILATU.......................MAREHEMU**

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO KWIMBA - MWANZA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI YA MIRATHI SIKU YA **IJUMAA TAREHE 06/08/2021** KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA . **MNADA UTAFANYIKA MAHALI MALI ILIPO.**

| S/N | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA, kiwanja na 30/31 kitalu "L" | MTAA WA UHURU, MWANZA. | SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATAILIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE KUANZIA TAREHE YA MNADA, KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0766-342969 / 0747405464**

RIPOTI MAALUM

# Kilichojificha hasara ATCL



Rais Samia Suluhu Hassan, akipunga mkono baada ya kupokea ndege mpya aina ya Bombardier DASH 8-Q400, iliyonunuliwa na Serikali ya Tanzania na kukodishwa kwa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), ilipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Sanula Athanas**

## ■Mkurugenzi ataja shida nne
## ■Rais Samia akiri, atasaidia

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), Ladislaus Matindi, ameweka mezani mambo manne yaliyolifunga miguu shirika hilo kupaa kuelekea kwenye uwanja wa faida.

Sambamba na kadhia hizo, serikali nayo imetangaza rasmi kupokea wito wa 'kulifungua miguu' ulioko katika mpango kazi wa shirika hilo ambao uko mbioni kufanyiwa mapitio ya kina kabla ya kuidhinishwa rasmi.

Hayo ni miongoni mwa mambo makuu yanayohusu undani wa kinachoendelea ATCL yaliyowekwa hadharani juzi jioni jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya mapokezi ya ndege mpya ya tisa iliyonunuliwa na serikali kwa ajili ya kutumiwa na shirika hilo.

Katika hafla hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan alipokea ndege hiyo aina ya Bombardier DASH 8-Q400 iliyotoka Canada, akikiri kufahamu kwa kina yanayotokea ndani ya ATCL na kuweka bayana kinachoendelea kuhusu kulifungulia njia shirika hilo.

**KIINI HASARA ATCL**

Katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Matindi, alisema hasara ambayo imekuwa ikiliandama shirika hilo imetokana na madeni yaliyorithiwa.

Alisema madeni hayo yamekuwa na athari kwa shirika kushindwa kuongeza mtandao wa safari na kuongeza hasara kwenye uendeshaji kutokana na riba ambayo nayo imekuwa ikichukuliwa kama gharama za uendeshaji.

"Tunashukuru serikali kwa kuchukua hatua kulipa baadhi ya madeni hayo yakiwamo madeni makubwa," Matindi alisifu.

Aliitaja sababu ya pili kuwa ni muundo wa umiliki wa ndege ambao unazifanya kuwa mali ya serikali, hivyo kuhusishwa na madeni ya serikali.

"Athari ya muundo huo ni kushindwa kutekeleza utanuzi wa mtandao wa ATCL, kutotanua mtandao kunaongeza hasara katika uendeshaji kwani matumizi ya ndege yanaendelea kuwa ya chini," alisema.

Mkurugenzi huyo alitaja sababu ya tatu kuwa ni muundo wa umiliki wa ndege kupitia mikataba ya ukodishaji kati ya ATCL na Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) ambao unaongeza gharama za uendeshaji na kuongeza hasara kwa shirika.

Matindi alisema mlipuko wa ugonjwa wa corona pia ni sehemu ya mzizi wa hasara, akifafanua kuwa ugonjwa huo umesababisha kupungua kwa idadi ya abiria wakati gharama za lazima za uendeshaji zikiendelea kuwapo.

"Hali hii imesababisha kuongezeka kwa hasara kama ilivyo kwa mashirika yote ya ndege duniani.

"Katika kipindi cha awali cha ufufuaji wa ATCL, serikali ilijikita katika kuanzisha shirika la kutoa huduma ya kulinunulia ndege, vilevile ilihakikisha kuna mifumo ya uendeshaji ya kuwezesha ndege hizo kufanya kazi.

"Jambo la muhimu katika uimarishaji wa ATCL ili iwe endelevu na shindani, ni kuhakikisha kampuni inaendelea kutoa huduma kwa tija kupitia ndege zinazohitajika kimkakati zaidi kibiashara na kiutalii kuiwezesha kuwa na miundombinu itakayopunguza gharama za uendeshaji ikiwamo karakana bora ili ndege zote zitengenezwe Tanzania," alisema.

Mkurugenzi huyo aliomba serikali kuirejeshea ATCL asilimia 20 za umiliki wa kampuni inayotoa huduma ya chakula kwenye ndege za serikali, akisisitiza uamuzi huo utawasaidia kupunguza gharama za uendeshaji.

Alisema ATCL imeongeza safari za kimataifa kutoka kituo kimoja cha Comoro hadi saba ambavyo ni Burundi, China, India, Uganda, Zambia, Zimbabwe na hivi karibuni inatarajia kuanzisha safari katika miji ya Kinshasa, Lubumbashi, Kalemie, Ndola, Nairobi, Dubai, Muscat na London.

**RAIS SAMIA**

Kwenye hotuba yake, Rais Samia alisema usafiri wa anga ni kichocheo muhimu cha maendeleo duniani kwa sababu usafiri huo ni wa haraka, salama na unotumiwa na watu wengi.

Alisema kuwa mbali na usafiri wa anga kusafirisha watu, pia ni muhimu katika kusafirisha bidhaa mbalimbali, hususan zinazoharibika haraka kama vile matunda, mboga za majani, samaki, maua na nyama.

Mkuu wa Nchi alisema serikali imeamua kununua ndege ya kusafirisha mizigo kwa sababu Tanzania ni miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa matunda, mboga za majani na maua.

Alibainisha kwamba mwaka 2019, Tanzania iliuza nje ya nchi mazao yenye thamani ya takriban Dola za Marekani milioni 700 na inatarajia kuingiza Dola za Marekani bilioni mbili kufikia mwaka 2025, yaani katika miaka minne ijayo.

Rais Samia alisema ili nchi iweze kuvutia watalii wengi na kunufaika nao ni lazima iimarishe usafiri wa anga na ndiyo sababu ya uamuzi wa serikali kuifufua ATCL ikiwa na malengo ya kupokea watalii milioni tano ifikapo mwaka 2025 kutoka watalii milioni 1.5 mwaka 2019.

Alisema serikali imeamua kuimarisha huduma za usafiri nchini ili inufaike na fursa za kijiografia za kupakana na nchi nane, ambazo kati yake, sita hazina bahari.

Rais Samia alizihimiza Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji na Sekta Binafsi kuweka mikakati ya kunufaika na fursa hizo ikiwamo kuanzisha kongani za kiuchumi kwenye maeneo kwa kuwa miundombinu ya usafiri inajengwa.

**MPANGO KAZI**

Rais Samia aliweka bayana kwamba katika miaka mitano ijayo, wanategemea kuliimarisha shirika hilo pamoja na sekta ya usafiri wa anga kwa ujumla.

Kuhusu vikwazo vinavyolikabili shirika hilo, Rais alisema serikali imepokea hoja zilizowasilishwa na Mkurugenzi Matindi na kuweka wazi Alhamisi alipokea mpango kazi wa shirika hilo.

Rais Samia alisema ofisi yake itaupitia na baadaye itakuwa na mjadala wa pamoja na ATCL na wizara husika kuona namna watakavyokwenda.

Pia alisema wanalifanyia kazi suala la hisa za ATCL kwenye kampuni inayotoa huduma ya chakula kwenye ndege hizo.

**HASARA ILIYORIPOTIWA**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mku wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2019/20 iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu, inabainisha serikali ilitumia jumla ya Sh. trilioni 1.028 kununua ndege nane kati ya tisa zilizonunuliwa awali.

Vilevile, katika ripoti hiyo, CAG Charles Kichere, anabainisha kuwa ndani ya miaka mitano kati ya 2015/16 na 2019/20, ATCL ilipatiwa ruzuku ya Sh. bilioni 153.711.

CAG anasema ndani ya kipindi hicho, ATCL ilipata hasara ya Sh. bilioni 153.542, huku ndani ya mwaka mmoja wa fedha (2019/20), ikipata hasara ya Sh. bilioni 60.246.

Kwa mujibu wa CAG Kichere, hadi kufikia mwaka huo wa ukaguzi (2019/20), ATCL ilikuwa na mtaji hasi wa Sh. bilioni 472.853.

HABARI KITAIFA

# TCRA yazindua mfumo wa leseni

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA), imezindua mfumo wa utoaji leseni kwa njia ya mtandao utakaochukua siku tano hadi 45 kwa lengo la kuongeza uwajibikaji, kuvutia wawekezaji na kupunguza urasimu.

Mfumo huo ulizinduliwa jana mkoani Dar es Salaam na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, kwa kushirikiana na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Innocent Bashungwa.

Dk. Ndugulile alisema kuwa hadi Septemba Mosi mwaka huu, TCRA inatakiwa iwe imekamilisha mapitio yote ili wawasilishe kwa Rais kwa ajili ya kuanza kwa utekelezaji.

"Tayari tumeshafanya maboresho katika suala zima la utoaji wa leseni, lakini bado mnatakiwa kufanya mapitio kwenye tozo na maudhui ya mtandaoni na namna ya kutekeleza, lengo ni kuhamasisha uwekezaji mkubwa," aliagiza.

Dk. Ndugulile alifafanua kuwa awali mfumo huo wa utoaji leseni ulikuwa ukichukua miezi hadi mwaka mmoja kukamilika lakini kwa sasa leseni ndogo hazitachukua zaidi ya siku tano na leseni kubwa chini ya siku 45.

Alisema wizara inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta hiyo ya mawasiliano na teknolojia ili kuzifikia wilaya 69 ambazo hazina redio nchini.

Waziri huyo alisema mfumo huo utamwezesha mteja kufuatilia kila hatua ya utolewaji wa leseni yake na utaongeza uwajibikaji kwa watendaji kwa sababu watakuwa wanaonekana wanavyotekeleza majukumu yao.

Waziri Bashungwa alisema mfumo huo utaondoa urasimu kati ya mteja na mtoa huduma kwa sababu maombi yatafanyika mtandaoni.

Alisema mfumo huo pia utaleta mabadiliko makubwa ya uendeshaji kwa sababu utaongeza weledi na ufanisi kwa wawekezaji kuomba leseni kwa ajili ya uwekezaji kwenye televisheni na redio.

"Mfumo huu unatutoa kwenye mfumo wa zamani wa kuwasiliana kati ya mteja na mtoa huduma uso kwa uso na sasa utaratibu utafanyika kwa sayansi na teknolojia na hata yale mambo mengine ya 'unanisaidiaje' (rushwa) hayatakuwapo," alisema Bashungwa.

Mkurugenzi wa Leseni na Ufuatiliaji TCRA, John Daffa, alisema mfumo huo utapunguza muda wa kuchakata maombi na kurahisisha utoaji wa leseni kubwa na ndogo.

Daffa alisema mfumo huo utaongeza uwajibikaji kwa mwombaji na mchakataji wa maombi kuhakikisha maombi hayo yanashughulikiwa kwa wakati.

# Polisi mbaroni tuhuma utoroshaji wa madini

**Na Mohab Dominick,**
KAHAMA

WATU saba, wakiwamo askari polisi wawili wanashikiliwa na Jeshi la Polisi Kituo cha Bugarama kwa tuhuma za kutorosha mawe matatu yanayosadikiwa kuwa na dhahabu.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Bulyanhulu, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Abdalah Kombo, alisema jana kuwa watu hao walikamatwa juzi majira ya saa sita usiku.

Alisema kuwa askari polisi na baadhi ya wachimbaji wa madini walikamatwa kwa tuhuma hizo.

"Ni kweli tukio hilo lipo, askari polisi na baadhi ya wachimbaji akiwamo meneja wa mgodi wanashikiliwa kwa kosa la kutorosha dhahabu lakini nisiwe msemaji sana, taratibu za kipolisi zinaendelea, itakapodhibitika, hatua za kisheria zitachukuliwa," alisema.

Ofisa Madini wa Mkoa wa Kahama (mkoa kisekta), Joseph Kumburu, akizungumza na Nipashe kwenye eneo la tukio, alisema watu saba wanashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kutorosha mawe yanayosadikiwa kuwa na dhahabu.

Alisema serikali imeingilia kati na kuhoji uongozi wa mgodi na mawe yaliyobakia yalioshwa na kupatikana na gramu 900.

Alisema kuna uwezekano mkubwa mawe yaliyopotea yana dhahabu nyingi na ndiyo sababu wanashikiliwa ili ijulikane yalikopelekwa.

"Namba ninayojua ya watu walioshikiliwa ni saba, wamo viongozi wa mgodi akiwamo meneja. Kuhusu askari, sina taarifa hiyo.

"Lakini, askari huenda walikuwa kazini, kwa maana hiyo lazima wakisikia kelele za wizi wanakwenda," alisema.

Mwenyekiti wa Mgodi huo wa Mbaga Patinas Gold Mine, Joseph Makoba, alikiri kutokea kwa tukio hilo lakini akasita kuwahusisha moja kwa moja askari polisi katika tuhuma hizo.

"Ni kweli kwamba usiku wa kuamkia juzi majira ya saa sita, zipo tuhuma za watu kudokoa dhahabu, kuanzia hapo tulivishirikisha vyombo vya dola na tukachukua hatua stahiki kuanzia kwa viongozi wenzetu katika mgodi.

"Baadhi ya watu wamechukuliwa na vyombo vya dola vinaendelea na uchunguzi na tutahakikisha tunashirikiana navyo ili kubaini nani anajihusisha na tabia hiyo mbaya," alisema Makoba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando, akizungumza na Nipashe kuhusu tuhuma za vijana kutorosha mawe hayo, alisema tukio hilo limeripotiwa kwake na amechukua hatua kadhaa.

"Nimeshamtuma RCO ili akachunguze tukio zima na baadaye kutalitolea ufafanuzi kwa vyombo vya habari.

"Kwa sasa ngoja kwanza uchunguzi ufanyike nitawapeni ufafanuzi mzuri baada ya kuletewa taarifa kamili juu ya tukio hilo kwani tayari nimemtuma RCO, naamini atafanya kazi nzuri, nanyi kupeleka ujumbe uliokamilika," alisema Kyando.




Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyika, akifungua rasmi utambulisho wa Mradi wa Uwezeshaji wa Vijana Wanaoishi na VVU Tanzania kushiriki mwitikio wa mapambano dhidi ya VVU katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe, unaotekelezwa na Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU (NACOPHA) kwa kushirikiana na NYP+ kwa ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (UNICEF), uliofanyika jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. Wanaoshuhudia ni Naibu Mtendaji Mkuu wa NACOPHA, Scholastica Williams na Mwakilishi kutoka UNICEF, Said Othman. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Vijana wachangamkie taaluma ya forodha'

**Na Christina Mwakangale**

CHUO cha Kodi (ITA) kimetoa wito kwa vijana kusomea taaluma ya forodha na kodi kutokana na uhitaji wa mkakati wa nchi katika kukuza mapato, uchumi na kupunguza utegemezi.

Ofisa Mkuu Uhusiano wa Umma wa chuo hicho, Oliver Njunwa, akizumgumza kwenye Maonyesho ya 16 ya Elimu, Sayansi na Teknolojia juzi, alisema ITA ni chuo pekee Afrika Mashariki na Kusini chenye ithibati ya mafunzo ya forodha na kodi.

Njunwa alisema kuna haja wanafunzi kusomea taaluma ya forodha na kodi kwa kujiunga na chuo hicho ambacho kimebobea katika kutoa taaluma hiyo kwa takribani miaka 14, akitamba kuwa wote watatoka na ujuzi.

"Tunawakaribisha vijana, wazazi, wananchi wote kupata maelezo ya kozi pamoja na kuwasaidia kutuma maombi chuoni. "Taaluma ya forodha inahitajika zaidi wakati Tanzania, ikiendelea kukuza mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi. Vijana wanaohitimu watasaidia kufanikisha lengo hilo," alisema.

Njunwa alisema wanafunzi hao watachagua kozi inayowafaa kutokana na sifa walizonazo na ambao hawajafikia vigezo vya kujiunga na ITA, wanaelekezwa katika vyuo vingine.

"Kwa wale wanaodhani kwamba ukisoma ITA lazima ufanye kazi Mamlaka ya Mapato (TRA), tunawaeleza kwamba kuna fursa nyingine nyingi za kufanya kazi ambazo mhitimu wa ITA anazipata.

"Anaweza kujiajiri mwenyewe kwa kufungua kampuni yake ya ushauri wa masuala ya kodi na akaajiri wengine, anaweza kuajiriwa katika taasisi za serikali, kwenye kampuni binafsi na hata katika mashirika yasiyokuwa ya kiserikali," alisema. Njunwa alibainisha chuo kinatoa mafunzo ya umahiri katika usimamizi wa forodha na kodi ngazi zote kuanzia astashahada, stashahada, shahada na shahada ya uzamili kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Muenster cha Ujerumani, katika sheria ya kodi na usimamizi.

Pia alisema mafunzo hutolewa ya muda mrefu na mfupi kwa taasisi mbalimbali pamoja na kufanya utafiti kuhusu masuala ya forodha na kodi ambayo husaidia nchi kutatua matatizo katika mifumo ya kodi.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaokaidi maagizo kujikinga na corona wachukuliwe hatua

**JANGA** la corona limeendelea kuisumbua dunia huku mamilioni ya watu wakiugua na wengine kwa maelfu wakipoteza maisha, jambo ambalo linasababisha athari za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Nchini Tanzania, kwa mfano, kila siku kumekuwa na taarifa za watu kufariki dunia katika maeneo mbalimbali kwa kile kinachodaiwa kuwa ni kutokana na changamoto ya kupumua huku hali ikiwa mbaya zaidi katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Iringa na Dodoma.

Katika Mkoa wa Kilimanjaro, mathalan, kumekuwa na taarifa za kusikitisha zaidi kutokana na ongezeko la vifo vya watu. Vifo hivyo si kwamba vinatokea katika mkoa huo pekee bali katika mikoa mingine na marehemu kwenda kuzikwa huko. Hii ni kutokana na utamaduni waliojiwekea watu wa huko kwa wengi wao kwenda kuzikwa nyumbani pindi wanapoaga dunia.

Ushuhuda juu ya hilo ni katika eneo la Mashati wilayani Rombo ambako ndani ya siku tatu, watu 21 wamezikwa huku sababu kubwa ya vifo vyao ikielezwa kuwa ni corona.

Kutokana na kasi hiyo ya vifo na watu kukumbwa na maradhi yanayoambatana na changamoto ya kupumua, serikali imechukua hatua za namna mbili. Ya kwanza ni ya watu kuchukua tahadhari na ya pili ni wananchi kuhamasishwa kuchanjwa huku kiongozi mkuu wa nchi, Samia Suluhu Hassan, akiongoza viongozi wa juu serikalini kupatiwa chanjo hiyo. Baada ya uzinduzi wa chanjo hiyo, tayari nguvu imeelekezwa katika sehemu mbalimbali mikoani huku vituo 550 vikiteuliwa kutekeleza suala hilo. Kwa upande wa hatua ya kuchukua tahadhari, serikali imeshatangaza afua juu ya kujikinga na corona zikiwamo kunawa maji tiririka na sabuni, watu kukaa mita moja kutoka mtu mmoja hadi mwingine, kuvaa barakoa na kuepuka mikusanyiko isiyo la lazima.

Sambamba na hayo, serikali imeagiza muda wa ibada kufupishwa kutoka ule uliozoeleka katika maeneo mbalimbali na vyombo vya usafiri kuhakikisha abiria wanakuwa kwenye viti tu na si kusimamisha.

Licha ya kutolewa kwa maagizo hayo, kwa kiasi kikubwa utekelezaji wake umekuwa mdogo kwa kuwa watu wanafanya mambo kama vile hakuna tatizo la corona. Kwenye vyombo vya usafiri, kwa mfano, katika Mkoa wa Dar es Salaam, watu wanajazana kiasi cha kukosekana sehemu ya kukanyanga mguu. Katika siku tatu zilizopita baada ya serikali kutoa maagizo, imeshuhudiwa watu wakiendelea kujazana kwenye mabasi ya daladala, mwendokasi na treni. Kwa ujumla, hakuna hatua zinazochukuliwa juu ya kujikinga na janga hilo huku askari wa usalama barabarani wakiwa wanaangalia bila kufanya lolote.

Mambo ya kujiuliza kutokana na ulegevu katika kuchukua tahadhari kwa upande mmoja na kutokuchukuliwa hatua wanaokiuka je, tunataka kusubiri kuona maafa zaidi yakitokea na nguvu kazi kupotea? Maagizo ya serikali kupuuzwa ni sahihi au viongozi wanaotoa maagizo hayo hawana meno kuwashughulikia wakiukaji?

Wahenga wanasema ukicheka na nyani mwisho utavuna mabua. Vivyo hivyo, kama hatua hazitachukuliwa ni dhahiri kwamba kuna uwezekano mkubwa taifa likashuhudia ongezeko la vifo vitokanavyo na corona.

Kama msemo kwamba kinga ni bora kuliko tiba, ni vyema hatua madhubuti zikachukuliwa kunusuru maelfu ya Watanzania, wakiwamo wale ambao ni nguvu kazi ya taifa dhidi ya janga hili ambalo limeigharimu dunia tangu kuibuka mwaka jana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wanafunzi hawa nao wanahitaji kujifunza mafunzo ya TEHAMA

**UKOSEFU** wa nishati ya umeme na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ni miongoni mwa mambo ambayo yamewahi kutajwa na serikali kuwa yanachangia kukwamisha ufundishaji wa somo la Teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Lakini ilishaahidi kufanya jitihada kuhakikisha kero hiyo inaisha, ili wanafunzi wa maeneo hayo wapate fursa ya kujifunza na kujua matumizi ya TEHAMA.

Kimsingi somo la TEHAMA linahitaji kuwapo kwa nishati ya umeme ikiwamo hata ya sola, ili iwe rahisi kulifundisha kwa vitendo, kwa maana ya kuwapo pia kompyuta na kuwafanya wanafunzi walielewe vizuri.

Hali hiyo inatokana na ukweli kwamba, ulimwengu wa leo wa utandawazi, matumizi ya TEHAMA yamechangia maendeleo ya sayansi na teknolojia kuzidi kusambaa.

Kwa hali hiyo, mwaka 2005, somo la TEHAMA lilianzishwa katika mtalaa mpya wa elimu ya msingi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ili kumpa mwanafunzi maarifa na stadi za matumizi ya habari.

Si hapo tu, bali pia somo hilo limsadie mwanafunzi awe wa mjini au vijijini, katika masuala ya vyombo vya mawasiliano, huku Kiswahili kikitumika kama lugha rasmi ya kufundishia somo hilo kwenye shule za msingi.

Lugha hiyo inatumika kama nyenzo ya kuwasilisha elimu ya sayansi na teknolojia kwa kisasa kwa wanafunzi, ingawa baadhi ya shule hazina nishati ya umeme, hali inayosababisha wanafunzi wasijifunze TEHAMA kwa vitendo.

Kwa kuwa ahadi ya serikali ni kwamba, hakuna kijiji kitakachoachwa bila umeme, basi umeme huo ungefika pia kila shule, ili kusaidia wanafunzi kusoma somo la TEHEMA kwa vitendo.

Hatua hiyo inaweza kuwasaidia wanafunzi wa shule za vijijini kutobaki nyuma katika somo hilo, ikilinganishwa na wenzao wa shule za mijini ambao shule zao zina nishati hiyo ikiwamo ya sola.

Ninatambua jitihada zinazofanywa za kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA), lakini itakuwa vyema iwapo nishati hiyo haitaishia katika nyumba za watu au katika maeneo ya biashara tu, bali hadi kila shule.

Hatua hiyo pia itawawia rahisi walimu kufundisha TEHAMA kwa vitendo iwapo shule zitakuwa na umeme. Wakati jitihada za kupeleka nishati vijiji zikiendeea, ni vyema pia kila shule kuwa na vifaa vya kufundisha somo hilo. Lakini pia ninaamini kwamba kuna shule nyingi tu ambazo hazina vifaa vya kufundishia somo hilo, hasa kompyuta, hivyo ili shule za vijijini zisionekane kama zinabaguliwa kwenye TEHAMA, nazo zipewe kipaumbele.

Hayo yakifanyika, wanafunzi wa shule za vijijini hawatakuwa nyuma kwenye somo hilo, hivyo si vibaya kushirikisha wadau mbalimbali wa elimu ili kuhakikisha shule za huko zinakuwa na nishati na vifaa vya kufundishia.

Wadau wa elimu wakishirikishwa, wanaweza kusaidia kupatikana kwa nishati hata ya sola na kompyuta kwenye shule hizo za pembezoni kwa kujitolea kichangia chochote ili kununua vifaa hivyo.

Njia hiyo pamoja na kuwajengea uwezo walimu wa somo hilo, kutokana na mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano duniani, wanaweza kufundisha vizuri na hivyo kuwafanya wanafunzi kupiga hatua kweenye TEHAMA.

Hiyo ni njia mojawapo ya kuwapo kwa mazingira rafiki ya ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo kwa shule zote nchini, bila kujali kwamba ni za vijijini au mijini, kwani wanafunzi wote wanahitaji kufundishwa.

Pamoja na hayo, ufundishaji wa TEHAMA kwa kutumia Kiswahili, binafsi ninaona ni vyema, kutokana na kwamba lugha hiyo inasaidia kujenga saikolojia ya kujiamini na kujithamini miongoni mwa wanafunzi.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Taifa limekubali chanjo, kupinga ni usaliti



Na Pascal Mayalla

**Tupaze sauti zetu zote ziwe ni sauti moja na tupambane bega kwa bega kwa mshikamano wa nguvu moja, sauti moja na lengo moja la ushindi. Hivyo ndivyo tutashinda vita hivi. Tukiendelea kupigana vita hii kwa hivi hivi tunavyokwenda sasa, kwa kila mtu kusema lakwake hatutoshinda.**

KUTOKANA na umuhimu wa chanjo ya corona kwa taifa na mapambano ya corona yanahesabika kama vita. Wiki hii nazungumzia umuhimu wa umoja na mshikamano kwa kutanguliza mbele maslahi ya taifa kuwa ndiyo siri pekee ya mafanikio ya vita vyovyote duniani.

Je, sisi Watanzania, serikali yetu, Chama cha Mapinduzi (CCM), wapinzani, viongozi wa dini, sekta binafsi na wote kwa umoja, kusimama pamoja kwa upendo, mshikamano na ushirikiano wa kupigana kwa pamoja kwa lengo moja, kwa nguvu moja, kwa sauti moja, ndiyo siri pekee ya mafanikio na kushinda vita hivi vilivyo mbele yetu.

Janga la corona ni vita, hivyo ili tushinde vita vyovyote ni lazima Watanzania tuwe kitu kimoja, tuwe wamoja tusimame pamoja kwa upendo na mshikamano kwa kufanya kila kitu kwa pamoja, kwa ushirikiano na kuwa kitu kimoja, kwa kuunganisha nguvu zetu zote ziwe ni nguvu moja ya pamoja.

Tupaze sauti zetu zote ziwe ni sauti moja na tupambane bega kwa bega kwa mshikamano wa nguvu moja, sauti moja na lengo moja la ushindi. Hivyo ndivyo tutashinda vita hivi. Tukiendelea kupigana vita hii kwa hivi hivi tunavyokwenda sasa, kwa kila mtu kusema lakwake hatutoshinda.

Tukipambana na virusi vya corona bila kusimama pamoja, huku kila mtu anasema lake, kama hali ilivyo sasa kwenye upinzani wa chanjo, Rais wetu Samia Suluhu Hassan baada ya kuchanja, ndivyo ametangaza silaha kuu ya mapambano, hivyo kiongozi yoyote wa umma, kupingana na msimamo wa Rais, msimamo wa nchi, huo ni usaliti. Kiongozi wa aina hiyo hapaswi kuvumiliwa hata kidogo.

Ili tushinde vita hivi, ni lazima kwanza viongozi wetu wazungumze kwa lugha moja na kutoa kauli moja thabiti na sauti moja, ili sisi Watanzania tufuate moja, tusimame pamoja kwa upendo na mshikamano. Tupigane pamoja, kwa nguvu moja, sauti moja na lengo moja. Kwa kufanya hivyo ushindi utakuwa dhahiri.

Ziko hatua ambazo tunapaswa kuzifuata katika kushinda vita hivi. Hatua hizo ni;-

**■ Ushirikishwaji**

Wakati wa vita vya Kagera, kabla ya kutangaza vita, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alituhamasisha, tukahamasika kwa uzalendo, ndipo akalihutubia taifa kutangaza vita na kusisitiza uzalendo na kujitoa. Umoja na mshikamano wa Watanzania wote kwenye vita hivi vya corona ndio msingi mkuu.

Mwanzo, serikali ndiyo ilihodhi ukamanda na wapiganaji wa vita hii, kwa kuunda kamati 3 za kiserikali tuu za kushughulikia corona. Lakini Rais Samia alipoingia, akaunda kamati nyingine ndogo na shirikishi kumshauri kuhusu Corona, ni ushauri wa kamati hii ndio uliopelekea Tanzania turuhusu Chanjo ya Corona

**■ Kauli moja**

Corona ni janga, ni vita na imeshatangazwa. Ili tushinde vita hii ni lazima viongozi wetu wa serikali, wanasiasa, wapinzani, wataalamu, wote tuzungumze kwa lugha moja, sauti moja na kauli moja iliyonyooka. Amiri Jeshi Mkuu au serikali ikiishasema jambo fulani, mfano sasa Tanzania tumekubali chanjo, haiwezekani wakati tuko vitani, linaibuka jitu linahamasisha tukaikatae!

Watu kama hawa wakiruhusiwa, tutawachanganya Watanzania. Kwenye hili lazima serikali, wapinzani wazungumze kwa lugha moja na kauli moja kwa maslahi ya taifa. Ile kanuni ya uwajibikaji wa pamoja ndipo inapotumika kwenye hili la corona. Tuongee kwa kauli moja, sauti moja na kupigana kwa nguvu moja na lengo moja na tutashinda.

**■ Viongozi wa dini, siasa kushirikishwa**

Tanakupongeza Rais Samia kushirikisha viongozi wa dini. Tumewashuhudia wakichanjwa ila hata wale wa aina ya Kibwetere si wa kuwapuuza kwani watakuja kutugharimu kama taifa, hivyo watafutiwe jinsi ya kuwaelimisha.

**■ Nafasi ya Wapinzani**

Upinzani katika hali ya kawaita unamaanisha kupinga, japo kisisasa ni jukumu la upinzani kupinga na kukosoa,. Hata hivyo, si lazima kupinga tu kila kitu na kila wakati. Linapokuja suala la maslahi kwa taifa, CCM na wapinzani wanapaswa kuweka tofauti zao pembeni na kuwa kitu kimoja.

Kwenye mazuri ya CCM kwa maslahi ya taifa, wapinzani wasione aibu kuiunga mkono CCM na kuipongeza. CCM nayo pia inapokutana na hoja za upinzani zenye maslahi kwa taifa, isione aibu kuwapongeza wapinzani kama hoja ya katiba mpya, elimu bure na kadhalika. Lakini inapotangazwa vita, nafasi ya wapinzani hubadilika. Hakuna tena kupinga kitu chochote! Zinatumika sheria za kijeshi, amri ni moja tuu, ama kuunga mkono au kunyamaza.

Haiwezekani Amiri Jeshi Mkuu au serikali ikasema kitu fulani halafu akatokea kiumbe mwingine akakohoa kuipinga serikali. Hili ni jambo la ajabu sana. Hii itakuwa si vita bali ni kusemezana. Kwenye vita hakuna kusemezana, ni amri tuu. Ikitolewa kauli yoyote rasmi ya serikali ni amri.

**■ Uzalendo**

Kwa vile mpaka sasa ugonjwa wa corona bado hauna kinga wala tiba, kilichopo ni chanjo na kuonyesha kuwa Watanzania ni wazalendo. Tusimame pamoja na Rais wetu na serikali yetu, tuwe kitu kimoja kwa kuunganisha nguvu zetu zote kwa pamoja chini ya umoja ni nguvu na ziwe ni nguvu moja kuu kweli.

Tupaze sauti zetu zote ziwe sauti moja na tupambane kwa mshikamamo, bega kwa bega kwa lengo moja la kushinda. Kwa pamoja tukachanje na tutashinda vita dhidi ya corona.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Ndoto ya babu inatafakarisha au siyo?



Na Joseph Kulangwa

**Walijiongoza vizuri, tena wakirithishana uongozi kwa kuzingatia busara, hekima na uwezo wa kiuongozi. Hawakuwa na kampeni za uchaguzi na vituko hivi na vile vya kupeana madaraka hata kama huna uwezo.**

NI ndoto. Nimelala mara naota babu ananitokea. Babu ananirudisha kwenye historia ya walimwengu. Ananiambia jinsi Wazungu walivyofika Afrika na mambo yao na kutulazimisha kuyafuata.

Ananisimulia kuanzia vyakula, dawa na tiba lakini pia imani za kidini. Ananiambia enzi zao vyakula walivipata shambani na si madukani. Nyama walichinja wenyewe hawakununua buchani au kwenye masupamaketi.

Babu anasema hawakuwa na hospitali walijitibia kwa mizizi na magamba ya miti hata majani. Joto la mwili wakilipima kwa mikono na si vipimajoto au themomita. Hawakudungwa sindano, ila walijichanja kwa nyembe za wakati huo.

Hawakuwa na masinagogi bali waliabudu chini ya miti mikubwa na miamba au mapango. Walitambika kuondoa mikosi. Ndivyo walivyoishi na wakaishi maisha marefu kuliko sisi leo tunaotikiswa na UVIKO- 19, na UKIMWI na kuhara na kuharisha!

Walijiongoza vizuri, tena wakirithishana uongozi kwa kuzingatia busara, hekima na uwezo wa kiuongozi. Hawakuwa na kampeni za uchaguzi na vituko hivi na vile vya kupeana madaraka hata kama huna uwezo.

Muda wote ananisimulia hataki nichomeke neno bali nisikilize kama nina swali ni baadaye. Na kweli anafunua ukurasa huu anafunika na mwingine na mwingine. Hatimaye anasema anaushangaa ulimwengu wa leo.

Akarudi Tanzania akaniambia Bunge lenu la leo si kama lile aliloshuhudia wakati anakaribia kukata roho. Akamuunga mkono Rais Samia kwamba wabunge wanademka, wameacha njia wanapita pembeni mwa njia. Wanakwepa masuala mazito wanajadili maskhara na utani. Kweli wanademka.

Nikamchomekea. Babu wewe kwa leo ungefanyaje? Anafunguka sasa; nchi yenu bado maskini hata kama mna uchumi sijui wa katikati. Mko maskini. Hamhitaji kuwa na Bunge la watu 400 leo huku idadi yenu bado ni milioni 60 tu! Mbona Marekani ina watu milioni 300 lakini wabunge 500?

Nikatoa macho nikajifanya nashangaa huku najua ndio ukweli. Akaendelea, ningekuwa mimi nina uwezo leo, nisingekuwa na Bunge, kwa sababu mfumo huo nao tuliletewa na wazungu wale wa Westiminsta!

Anasema ningeteua watu 30 tu, watu hao wawe ni wastaafu kutoka fani mbalimbali tofauti, mathalan majaji au wanasheria nguli, wakuu wa vyuo mbalimbali galacha na wengineo waliotukuka katika fani na tasnia zao.

Hao kwa umri wao na busara na hekima zao ndio wangeunda Bunge ambalo lingekuwa linakutana kila miezi mitatu na kututungia sheria mpya na kurekebisha au kufuta zilizopitwa na wakati, ili mradi kuwa na sheria rafiki ambazo zitamwezesha kila mtu kufanya yake bila kuzivunja.

Wastaafu hao kwa kuwa wanapokea pensheni zao, ningekuwa nawalipa posho za kikao cha Bunge hata kama ni milioni kwa siku, lakini zisingefika hizi tunazopoteza leo kwa baadhi ya wanaodemka tu wakisubiri sijui Sh. milioni 200 baada ya kumaliza miaka mitano!

Anasema angeteua mawaziri wenye weledi katika maeneo watakayoyaongoza na si kuwekwa tu kwa sababu nawafahamu au ni watoto wa skulimeti wangu au kolejimeti wangu la hasha! Hao wangebanwa na Bunge hilo la wazee wenye hekima mpaka wangeacha midemko!

Ananiambia babu, kwamba hata asingekuwa na haja ya wakuu wa mikoa wala wa wilaya, ila angehakikisha kila kata ina mtu makini anayeweza kusimamia eneo lake, huku akiwasiliana moja kwa moja na waziri mhusika, ili kutatua tatizo na kusonga mbele. Ingepunguza hata matumizi.

Akataka kurudi kwenye mawaziri, eti amesahau nikamwambia babu songa mbele karibu kunakucha na ndoto hairudii. Akasema basi lakini akagusia tu kuwa wizara angepunguza sana pengine ziwe nusu au robo ya wabunge. Eti nyingi zinaingiliana majukumu. Akaniahidi usiku mwingine.

Mara nikasikia nagongewa mlango eti kumekucha natakiwa kwenda kutumika kibaruani. Naruka kitandani huyo maliwatoni. Nabaki najiuliza sasa hivi babu haya ni ya kweli? Kwa mbali naona kama babu anatafakarisha. Tuache kudemka ,tuchape kazi na iendelee au vipi?

**Alamsiki!**

SAFU

KONA YA UKWELI

# Ripoti ya LHRC iwape somo waajiri kuacha manyanyaso



Na Thobias Mwanakatwe

JULAI 29, 2021 itabaki kuwa kumbukumbu katika historia ya Tanzania baada ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kuzindua ripoti ya Haki za Binadamu na Biashara ya mwaka 2020/21.

Uzinduzi huo ambao ulifanyika katika ofisi za LHRC, Dar es Salaam na utafiti wa ripoti hiyo ulilenga kuagalia biashara inaheshimu vipi haki za binadamu. Mikoa 15 ilifanyiwa utafiti kwa kupita katika taasisi za udhibiti, kampuni, wafanyakazi na madereva.

Uzinduzi huo ulioshuhudiwa na watu kadhaa, wakiwamo mabalozi wa nchi mbalimbali kupitia mtandao wa Zoom, moja ya mambo ambayo yalijitokeza ndani ya ripoti ni suala la uonevu na vitisho kwa waajiri katika sehemu mbalimbali za kazi. Jambo hilo lilitajwa kuwa ni ukatili wa kijinsia ikifuatiwa na unyanyasaji wa ngono.

Ripoti ilibainisha kuwa asilimia 29 ya wafanyakazi waliohojiwa walikiri kukutana na unyanyasaji wa kijinsia maeneo yao ya kazi. Kati ya waliohojiwa, asilimia 73 ulikuwa ni uonevu na vitisho na asilimia 15 wakiripoti unyanyasaji wa kingono.

Ilibainisha pia kuwa asilimia 62 ya wafanyakazi wamekuwa wakifanya kazi kwa muda wa ziada bila malipo, kupewa malipo kidogo na kutopewa mikataba ya kazi.

Ofisa Mwandamizi wa Kitengo cha Utafiti LHRC, Fundikira Wazambi, akabainisha kuwa pamoja na kuwapo kwa unyanyasaji na ukatili huo kwa waajiriwa, bado walio wengi hawana uelewa wa sheria za kazi na haki zao.

Mfano suala la likizo ya wazazi kwa wanawake limekuwa changamoto sana ambapo ripoti ilibainisha kuwa baadhi wamepoteza kazi kabisa.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema katika utafiti huo jambo lingine lililobainika ni mikataba ya ajira. Asilimia 59 ya wafanyakazi wengi walioshiriki walisema wana mikataba ya ajira kiwango ambacho kimeshuka ukilinganisha na hali ilivyokuwa mwaka jana.

"Idadi ya wafanyakazi wenye mikataba ya ajira ni pungufu kwa asilimia 25 ukilinganisha na idadi ya wafayakazi weye mikataba hiyo katika utafiti uliopita wa mwaka 2019 ambapo asilimia 84 walidai kuwa na mikataba ya ajira," anasema.

Akasema utafiti huo pia umebaini ombwe la kukosekana kwa uelewa juu ya sheria za kazi na ajira baina ya wafanyakazi. Mkoa wa Tabora ndio ulioongoza kwa kuwa na asilimia kubwa zaidi ya wafanyakazi wasio na uelewa wa kutosha kuhusu sheria na kanuni za kazi.

Nianze kwa kusema kuwa waajiri watambue kuwa mwajiri haikufanyi kuwa juu ya sheria. Sheria zipo kumlinda mfanyakazi, hivyo hakuna sababu ya kumnyanyasa. Kujenga uhusiano mzuri na wafanyakazi ni jambo ambalo kwanza linaongeza ufanisi wa kazi lakini mwajiri anamponyanyasa wafanyakazi hata ufanisi wa kazi unashuka.

Kwa mujibu wa Ibara ya 12 na 13 ya Katiba ya Tanzania, watu wote wanazaliwa sawa na wako sawa mbele ya Sheria. Aidha, Katiba inatambua haki ya kupata kazi na haki ya kupata malipo stahiki (Ibara ya 23).

Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya mwaka 2004 pia inamtaka kila mwajiri kuhakikisha kuwa wanaume kwa wanawake aliowaajiri wanapata malipo sawa kwa kazi zenye thamani sawa wazifanyazo.

Aidha Ibara ya 13 ya Katiba ya Tanzania, inakakataza ubaguzi wa aina yoyote kwa minajili ya utaifa, udini, mahali pa kuzaliwa, mwelekeo wa kisiasa, rangi, dini au kazi aifanyayo mtu. Sheria ya kazi pia inakataza ubaguzi katika nyanja za rangi, utaifa, mahali pa kuzaliwa, jinsia, ujauzito, hali ya kuoa au kutooa, asili ya mtu, mwelekeo wa kisiasa, ulemavu au UKIMWI.

Haitachukuliwa kama ubaguzi pale ambapo hatua madhubuti za kusaidia kukuza ajira kwa kundi liliosahauliwa au ambalo limekuwa likibaguliwa kwa muda mrefu katika soko la ajira; kama vile kupendelea, kutenga au kuchagua mtu yeyote kwa minajili hii ya kazi, au kuajiri wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Ajira.

Nimalizie kwa kusema waajiri waheshimu sheria na kuacha kufanya manyanyaso kwa wafanyakazi wao na ripoti hii ya LHRC ifungue ukurasa mpya kwa waajiri kubadilika kuwa rafiki wa wafanyakazi badala ya kuwa adui.

Niwapongeze LHRC na wadau wote waliofanikisha kufanyika kwa utafiti wa ripoti hii na hivyo ni wajibu wa serikali kuhakikisha wanafuatilia kuona utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na LHRC yanatekelezwa.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU IBARIKI LHRC.**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

DARASA LA NDOA

# NAMNA YA KUEPUKA WAKWE NA NDUGU KUINGILIA NDOA - 1



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

WIKI mbili zilizopita mfululizo, tuliangalia kwa kiasi gani baadhi ya mambo yanayosababisha ndugu na wazazi kuingilia ndoa na hatimaye kusababisha wanandoa washindwe kuchukua zipi katika kunusuru ndoa pale tatizo linapojitokeza.

Miongoni mwa hatua hizo husababisha baadhi ya wanandoa huchukua hatua ambazo hatimaye huwadhuru wenyewe, lakini wakati mwingine huyaacha mambo yaende yalivyo. Hii nayo haileti suluhisho kwa kuwa wanaoingilia ndoa hushinda na kuwaacha wanandoa wakiwa na maumivu makubwa.

Hata hivyo, ni muhimu kujua namna tunavyoweza kujitoa kwenye kero hii. Kuna njia mbalimbali ambazo tukizitumia tunaweza kuzuia uwezekano wa kujikuta tunavurugana na wakwe au ndugu wa waume au wake zetu na kutoka kwenye tatizo hilo.

Ni vigumu kutaja zote, bali naamini zifuatazo ndizo kubwa:

Mawasiliano mazuri

Mume na mke huzungumza, lakini hawawasiliani. Kuzungumza ni kubadilishana kauli au mmoja kusema na mwingine kusikiliza, wakati kuwasiliana kuna maana ya wanandoa kusema hisia zao, kusikilizana na kufikia mwafaka wa yale yote yanayowagusa kwenye maisha yao ya kila siku.

Kama tulivyoona katika makala ya mawasiliano kwa wanandoa, kuna ngazi tatu za mawasiliano. Kuna wanandoa ambao kwa bahati mbaya hawajafikia hata kwenye ile ngazi ya awali ya mawasiliano. Kwa hawa, si tu kwenye suala la kuingiliwa kwenye ndoa, bali hawawezi kufanikiwa kuwa na uhusiano au ndoa imara naya kudumu.

Kwenye mawasiliano ya kindoa, ngazi ya pili ni ile ambapo mnaweza kujadili masuala yenu na ya ndugu zenu au wazazi ambayo yanawagusa wote. Kama hakuna mawasiliano kwenye ndoa yenu, wazazi au ndugu wanaweza kuichezea ndoa hiyo kwa kadiri wanavyotaka.

Iwapo tunataka kuzuia uwezekano wa wazazi au ndugu zetu kuingilia ndoa zetu, hatuna budi kuwa na mawasiliano ya wazi na moja kwa moja kati yetu. Linapotokea jambo ambalo tunaliona lina mwelekeo wa kuingiliwa kwa ndoa yetu, inabidi kulitafutia jambo hili ufumbuzi wa kudumu kwa pamoja. Kama kila mmoja atakuwa mkweli kwenye suala hilo ni lazima mawasiliano yatazaa matunda.

Kuwa mkweli ina maana ya kujadili bila kupendelea au kuonea upande wowote, kwa lengo la kuleta amani na upendo zaidi kwenye ndoa. Endapo mmoja kati ya wanandoa atakuwa na ajenda ya siri, mjadala au mawasiliano ni lazima yatakwama.

Mume asijaribu kumtetea mzazi au ndugu yake hata pale ambapo wazi anaona ana makosa. Mke naye asijaribu kutafuta mbinu ya kumkosanisha mumewe na wazazi au ndugu zake. Kila mmoja ajitahidi kujali maslahi ya ndoa na siyo maslahi au utashi binafsi.

Tumezungumzia vibandiko hapo kabla. Hii ina maana kwamba wanandoa wanapojadili kuhusu ndugu na wazazi wao, wasiweke vibandiko vya u-baba, u-mama, u-dada, u-kaka na u-shemeji. Kila mmoja amchukulie mzazi au ndugu wa mwanzake kama mzazi au ndugu yake. Hii inaweza kuleta mafanikio makubwa sana katika kuwezesha wanandoa wasiingiliwe kwenye ndoa yao. Kunapokuwa na vibandiko, kunakuwa na mipaka ambayo itafanya wanandoa kushindwa kukutana kihisia na kimaamuzi kuhusu wazazi au ndugu wa kila upande.

Wanandoa wajifunze kukua

Mtu akiwa ameoa maana yake ni kwamba, amekua mtu mzima mwenye uamuzi. Hivyo, mwanandoa kusubiri kuambiwa afanye nini au kufuata kila kitu wazazi au ndugu wanachotaka au wasichotaka ni kuikosea ndoa hiyo na matokeo yake ni misuguano na ugomvi ndani ya ndoa, kwani nafasi ya mwenzi inakuwa haipo tena.

Ikumbukwe kuwa, wazazi wetu au ndugu zetu hawana tofauti na watu wengine wowote kwenye jamii au duniani. Hata sisi huenda tu wazazi pia. Hii inaonesha kwamba, kuwa mzazi haina maana ya mtu kuwa na thamani zaidi ya mwingine. Sifa ya awali ya kila binadamu ni ubinadamu wake, hizo sifa nyingine za u-baba, u-mama, u-dada au u-kaka ni vibandiko vya kibinadamu, kimantiki hazina maana kubwa kwa kiwango ambacho zinapewa.

Baba au mama, kaka au dada wanastahili kuheshimiwa nasi kama binadamu kwanza, halafu kama ndugu au wazazi. Lakini kuwa ndugu au wazazi hakuwapi watu hawa haki wala mamlaka ya kuingilia ndoa za watoto wao. Pamoja kwamba mtoto hakui kwa mzazi, inapofikia hatua ya ndoa, kuna mipaka ya kutunzwa na kuheshimiwa na wazazi ili ndoa ikue.

Kukua ni pamoja na kujua kwamba, hata mzazi anaweza kukosea kama binadamu mwingine yoyote. Mzazi anapoanza kutoa amri au kuingilia ndoa yako, usimtazame kama mzazi tu, bali kama binadamu. Ukimtazama kama binadamu utaona udhaifu wake na utakuwa tayari kuukabili. Kama mzazi atatumia kibandiko chake cha u-baba au u-mama kutaka ufanye ayatakayo wakati unajua siyo ya haki wala kujenga, bali yanatokana na udhaifu wake wa kibinadamu, ni muhimu kupingwa kwa hekima kwa nguvu zote kwa maslahi ya ndoa yako.

Kuna wazazi ambao wakipingwa hutishia kutoa laana. Ukweli ni kwamba, kama tatizo ni mzazi, laana hiyo itamrudia mwenyewe. Unachotakiwa kufanya ni kuonesha msimamo, kupinga kwa ustaarabu na upendo na kuonesha kwamba, nawe umekua, hasa pale yanapojitokeza mambo yenye muelekeo wa kubomoa badala ya kujenga ndoa.

■ **Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

Agosti 1, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




HARUSI YAKO INAKUWA NA FURAHA ZAIDI KAMA IKIWA NA VIONJO VINGI VITAMU, VIJANA HAWA WA KUNDI LA J4 WASAFI MAIDS, KUTOKA MKOANI MWANZA, WANASIFIKA KWA KAZI YAO NZURI YA KUSINDIKIZA MAHARUSI NA KUIFANYA SHEREHE KUWA YA KIPEKEE.

## HARUSI

Ukurasa 12

Ukurasa 15



## MAISHA NI NYUMBA

### Usijenge nyumba kwenye udongo wa mfinyanzi

### Namna ya kukaanga nyama bila mafuta




Ukurasa 14




## TUPIA MTANDIO

# UPE JOTO MWILI, NG'ARISHA MWONEKANO


Ukurasa 13





## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
EVA, VUA, SIE, AGO,
LETU, VUKA, STAILI, MAKATO








## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO



SWALI
Samaki aina ya papa wanapatikana wapi?

MTOTO mmoja alikuwa akicheza na wenzake, mara mvua ilianza kunyesha na wote walianza kushangilia na kuoga. Wakati wakiendelea kuoga maji ya mvua, mama yake alitokea na kuanza kumuonya.

Mama; Kwa nini mnacheza kwenye mvua?

Mtoto: Tulikuwa tunacheza, mara mvua ikanyesha tukajikuta tunaoga?

Mama: Maji ya mvua si mazuri kiafya

Mtoto: Mbona wewe uliniambia mvua sawa na neema?

Mama: sawa, lakini .....

Mtoto: Kama neema na sisi tuache tushangilie.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Hekima inavyoweza kunusuru ndoa iliyogubikwa na mtikisiko

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Bado darubini inamulika wale wanawake wanaowafanyia visa waume zao pasipo sababu za msingi.
Mungu amewapa waume wapole, wachakarikaji lakini wao wanawanyanyasa na wakati mwingine kuwapiga jambo ambalo si sawa. Wiki iliyopita nilimjadili mama mmoja ambaye alikuwa hajali familia yake.
Yeye akitoka kwenda kwenye kazi yake ya ushonaji wa nguo, anarudi usiku huku watoto wakimsubiri nje baada ya kurejea toka shuleni. Tabia hii ilifikia hatua mama mkwe (mama mzazi wa mume) kuamua kuwachukua watoto hadi mgogoro wa wanandoa hao kupatiwa ufumbuzi.
Mume wake ni mfanyabiashara, anaipenda familia yake lakini mke ndiye kiruka njia. Alipochunguza nyendo za mkewe kwa nini anachelewa kurejea nyumbani, akagundua yuko dowezi anayeingilia ndoa yake.
Mpenzi msomaji, vituko vya baadhi ya kinamama kutesa waume zao vipo vingi. Hebu sikia na hiki kingine kisha mwishoni nitatoa tafsiri ya mke na ushauri.
Yuko baba mmoja alikuwa akimsimulia shemeji yake mkewe anavyomtesa na hatua ambazo amedhamiria kuzichukua ili kujiokoa. Akasema, anaipenda familia yake ya mke na watoto wawili. Lakini kwa mateso haya ameinua mikono juu.
Baba huyu ana watoto wawili, mkubwa miaka sita na mdogo miaka miwili na nusu. Ndoa yao imedumu miaka saba sasa lakini anasema mkewe ni mkorofi kila mara ni ugomvi.
Lakini kwa bahati mbaya wote ni wanywaji wa pombe, hivyo mizozo mingi ni baada ya kupiga ulabu (pombe) .
''Mimi ni mfanyabiashara, mke wangu ni mwajiriwa serikalini. Lakini tatizo ni mke wangu kunionea na kunipiga kila wakati. Kuna wakati nilivunjika mkono wakati nikijitetea.
''Ndani ya nyumba hamna amani. Hata ndugu zangu hawapendi anawasema vibaya dada zangu, jambo ambalo linaniumiza sana. Hivi sasa najipanga nipate mahali salama pa kuishi. Nachoka kusimangiwa nyumba tunayoishi ambayo kiwanja alitafuta yeye na sehemu kubwa ya ujenzi amechangia yeye.
Hilo nalo ananisimangia sana hadi Napata kizunguzungu.
Anasema huwa anafikia mahali anaondoka hata wiki, mkewe anamtafuta na kumsihi arudi watoto wanamwulizia. Hata anaporudi hazipiti siku mbili analianzisha tena.
''Kiukweli nimechoka, najipanga nikatafute hifadhi tulivu. Maisha bila amani siyo maisha'', ndivyo anavyomalizia kusema kijana huyo.
Mpenzi msomaji, bila shaka umemsikia vema kijana kwa yanayomsibu. Hebu tuone tafsiri ya 'mke'. Mke ni mwanamke aliyeolewa. Tuone aina za wanawake.
Wapo wanawake wenye upendo ambao ni wavumilivu na huweza kuchukuliana na kila hali. Pia wako wanawake wakorofi wasiotaka kushuka hata kama wamekosea. Wanawachukia wakwe na mawifi bila hata sababu ya msingi.
Wengine huwalaumu wakwe zao wakati hawana tatizo lolote. Wanawake wengine wana tabia mbaya kiujumla pengine kutokana na asili ya kwao. Tabia zingine ni za kurithi na zimetesa wengi pasipo wao kujua.
Msomaji wangu, wiki iliyopita nilisema kila mwanamke mwenye hekima hujenga nyumba yake, bali mpumbavu huibomoa kwa mikono yake mwenyewe. Ni dhahiri kwamba kama mke ndani ya nyumba, anaweza akajenga msingi imara wa ndoa yake kwa kutumia hekima na maarifa.
Hata hivyo, ni muhimu kutambue kuwa inahitajika hekima ya Mungu kuujenga ulimwengu. Na hauhitaji chochote ila hekima kujenga nyumba yako.
Mwanamke hatakiwi kuropoka ovyo bali kuwa na hekima ya kuongea na pia ushirikiano wa kinywa chake kabla hajaongea chochote.
Kama mwanamke atakuwa na hekima ataweza kumchunga simba, lakini kama hana hekima kwenye kinywa chake hata kondoo atashindwa kumchunga. Amri ya Mungu inaagiza mwanamke amtii mume na akishindwa kumtii hata yeye hatakaa atii kile anachotaka amfanyie.
Pia mwanamke anapaswa kuwa makini kwa yale anayomtamkia mumewe na hata juu ya familia kwa maana wanaweza kutumia maneno ya kinywa chako kukushambulia. Hata kama mume au wakwe au ndugu za mume wamekukasirikia, kuwa na hekima, badilisha tabia yako na uwezo wa kutawala kinywa chako.
Tunza nyumba yako kwa kufunga mdomo wako. Uwe mwangalifu usije ukajiandalia talaka kwa kufungua kinywa chako. Jifunze kunyamaza na Mungu atakuongoza.
Ndoa zirejee upendo wa kwanza ili zidumu. Niishie hapa tukutane wiki ijayo. Je, una maoni, kisa? Tuma ujumbe 0715268581 .

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Wenye ushawishi kwenye jamii wasipotoshe wananchi kuhusu chanjo

MJADALA mkubwa miongoni mwa Watanzania ni kuhusiana na chanjo ya corona iliyowasili na kuanza kutolewa nchini kwa makundi maalum yakiwamo ya viongozi wa juu serikalini na wenye umri wa zaidi ya miaka 50, wagonjwa na vyombo vya ulinzi na usalama.

Chanjo hiyo inatolewa kwa hiari kwa kila atakayekuwa tayari kuchanjwa na anatakiwa kutia saini kuwa amekubali kwa hiari yake.
Serikali ilieleza umma kuwa imepokea chanjo milioni moja ambazo ni aina ya Johnson and Johnson ambayo imeorodheshwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kati ya chanjo sita zinazotumiwa na nchi mbalimbali duniani.

Ziko taarifa nyingi ambazo zinazungumzwa na baadhi ya viongozi wa kijamii wenye wafuasi wengi ambao wameamua kujivika utaalam kiasi cha kushawishi wananchi kukataa chanjo kwa sababu mbalimbali ambazo wao wanaamini pasipokuwa na utafiti wowote wa kupinga chanjo hiyo.

Viongozi hao ni baadhi ya wanasiasa, viongozi wa dini na kijamii ambao kwa uamuzi na mtazamo wao, wameweka msimamo hadharani kuwa hawatachanja na sasa pasipokuwa na uthibitisho wa kisayansi wanataka wananchi kutokubali maelekezo ya serikali.

Kwanza, ieleweke kwamba tangu kuingia kwa mfumo wa digitali, upatikanaji wa taarifa umerahisishwa kiasi cha mtu mwenye simu janja na mgando anaweza kutuma na kupokea taarifa yoyote lakini wajibu wa kuchuja kipi aamini na kipi aache ni wake mwenyewe.

Corona ni janga la dunia na ziko nchi zimeanza mapema sana kuchanja watu wao.
Nchi kama Marekani imefikia hatua inawalipa raia wake Dola za Marekani 100 kwa kila atakayekwenda kuchanja. Yote hii ni katika kutaka wawe salama.

Ziko nchi zimefanikiwa kuchanja watu wake kwa asilimia 90 na idadi ya wagonjwa na walio mahututi au vifo vimepungua kiasi cha huduma za afya kupumua kwa kuwa awali vilielemewa na wagonjwa.

Wengine wamerudi kwenye shughuli zao kama kawaida kwa kuwa wamefanikiwa kuchanjwa na wanajitahidi kwamba kila mtu achanjwe ili kukabili kirusi hicho kinachobadilika muundo kila wakati.

Wataalam wa afya, ikiwamo WHO, wameeleza bayana kuwa kuchanja kunapunguza uwezekano wa kupata corona kali, kuendelea kusambaza, kuzidiwa na vifo na wengi wana uwezekano wa kupata lakini wakapona kuliko ambaye hajachanjwa.

Wanasema ugonjwa huo hushambulia sana sehemu ya chini ya mapafu na wengi wamefika hospitali wakiwa katika hatua mbaya huku wengine wakitumia dawa za kienyeji ambazo kutokana na kutokuwa na kipimo sahihi, wameathirika zaidi.

Kwa sasa serikali inasema wazi kuwa baadhi ya hospitali zimeelemewa na vifo vinaongezeka na msisitizo mkubwa ni kuchukua tahadhari huku mwongozo umeshatolewa kwa makundi yote namna ya kukabili maambukizi ya virusi hivyo.

Tatizo kubwa ni kirusi kubadilika badilika kwa kuwa kilichovamia awali si kinachovamia sasa na sasa tupo kwenye wimbi la tatu huku nchi jirani ya Kenya ikiwa katika wimbi la nne na yote yanawatesa sana.

Jana, Kenya ilitangaza kuwa hospitali za umma zimeelemewa na wagonjwa kiasi cha kuangakia uwezekano wa kuongeze wodi za wagonjwa mahututi.

Hali ni ngumu kwenye nchi nyingi hasa kwa namna kirusi hicho kinasambaa kwa kasi, jambo linaloonyesha kuwa chanjo haikwepeki na ni suala la muda tu kukamilisha.

Ni muhimu sana kila mmoja kusikiliza wanachosema wataalam na kufanya uamuzi binafsi kwa kuwa suala la afya ni la mtu binafsi na si shirikishi.

Haipendezi kwa baadhi ya watu wenye ushawishi kutumia nafasi zao kushinikiza wengine wasikubali chanjo hiyo huku baadhi wakidaiwa walishapata chanjo nje ya nchi jambo ambalo si sawa kabisa.

Tusikilize wataalam wa afya wanasemaje na kuchukua hatua, lakini ni muhimu kasi ya utoaji elimu ikaongezeka ili kuokoa watu ambao wanaweza kujiepusha na kuchukua hatua.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene amesema idadi ya vifo ni kubwa huku akitolea mfano kuna nyumba moja ya ibada ilizika watu 21 kwa siku tatu.

**Mungu ibariki Tanzania.**



**HARUSI YAKO INAKUWA NA FURAHA ZAIDI KAMA IKIWA NA VIONJO VINGI VITAMU, VIJANA HAWA WA KUNDI LA J4 WASAFI MAIDS, KUTOKA MKOANI MWANZA, WANASIFIKA KWA KAZI YAO NZURI YA KUSINDIKIZA MAHARUSI NA KUIFANYA SHEREHE KUWA YA KIPEKEE.**





Tunachapicha picha za harusi bure wasiliana kwa namba 0717336368, au barua pepe: Moshilusonzo@ Gmail.com" Moshilusonzo@Gmail.com.



# MITINDO

## TUPIA MTANDAO

# UPE JOTO MWILI, NG'ARISHA MWONEKANO







WAKATI wa msimu wa baridi kila mtu anatumia mavazi yake kujikinga pamoja na kuongeza mvuto wa mwonekano wake wa nje.

Mitandio ni baadhi ya mavazi yanayotumika sana kuhifadhi na kuongeza joto sehemu ya shingo, lakini vazi hili linanogesha kwa kuongeza uzuri wa mtumiaji.

Aina hii ya kitambaa inachukuliwa kama vazi maarufu la nyongeza katika msimu wa baridi. Kuna aina mbalimbali ya uvaaji wa mitandaio inayofaa kuvaliwa katika kipindi hiki.

SHAWL

Ni aina ya mtandio ambao unapendwa kutokana na mwonekano wake. Wanawake wengi wanapenda vita vyepesi vilivyotengenezwa kwa uzi wa Hariri, Silva au pamba.

PALATINE

Mwonekano huu wa kipekee unatokana na kitambaa kizito cha blanketi, huwapendezesha wanawake pale wanapoweka shingoni. Wabunifu wameongeza vionjo kwa kutengeneza ya manyoya na mapambo mengine ya kupendeza.

SNOOD

Snood ni mtindo uliopata umaarufu katika kipindi kifupi, inachukuliwa kama mtandio rahisi zaidi na imetengenezwa kwa pamba, manyoya na ngozi.

# UREMBO: MAFUTA YA MAWESE

# Furahia ngozi laini inayoita



MAFUTA ya mawese yanajulikana na wengi kama kiungo kizuri cha chakula, lakini yana umuhimu mkubwa katika kujenga na kuimarisha afya ya ngozi.

Kutokana na kuwa na utajiri wa viini lishe, kampuni mbalimbali ya vipodozi wamejikuta wakipigana vikumbo kubuni na kuzalisha bidhaa tofauti zenye mafuta hayo.

Ukipita madukani utakuta kuna sabuni, shampoo na mafuta ya mawese kwa ajili ya matumizi ya urembo. Hii ni kwa sababu ya ubora wake na kuwa suluhisho katika maswala yanayohusu afya ya ngozi.

**SIRI NDANI YA MAWESE**

Kama ilivyo kwa mafuta mengine halisi, mafuta ya mawese ni bora kwa kuwa na virutubisho ambavyo ni asilia.

VITAMINI E

Mafuta ya mawese yana vitamini E, inayofahamika kama tocotrienols ambayo imefanyiwa utafiti na kugundulika inakinga ugonjwa wa saratani, matatizo ya ubongo na moyo.

Tocotrienols pia inasaidia kukinga ngozi na miale ya jua na kupunguza alama ya makovu.

**VITAMINI K**

Vitamini K inasaidia ngozi iweze kuwa na uwezo zaidi wa kujitibu yenyewe pale mtu anapopata majeraha na kupona haraka.

Pia kiini lishe cha Glycolipids, inasaidia kuifanya ngozi kung'aa na kuirudisha katika ujana. Mafuta haya yanasaidia ngozi kulainika na kuondoa makunyazi ya uzee.

# MAPISHI

Na Mary Geofrey

# NAMNA YA KUKAANGA NYAMA BILA MAFUTA



NYAMA ya ng'ombe inapendwa na watu wengi na kuna aina mbalimbali za mapishi yake, leo tutaelekezana namna ya kukaanga bila kuweka mafuta.

**Maandalizi**

Nyama nusu kilo, tangawizi ya unga kijiko kimoja, mafuta ya kula, kitunguu maji kimoja kata vipande, limao moja na kitunguu saumu punje tano.

Mahitaji mengine ni pilipili hoho mbili, chumvi kijiko kimoja, pilipili manga ya unga kijiko kimoja.

**Namna ya kupika**

Baada ya kukatakata nyama yako, paka chumvi pande zote za nyama, nyunyizia limao, tangawizi, kitunguu saumu kilichopondwa.

Paka vizuri pande zote hadi zienee, weka pilipili manga, paka vizuri na acha nyama ikae pembeni iingie viungo kwa dakika 10 hadi 15.

Bandika kikaango jikoni, acha kipate moto kiasi, weka nyama, zipange ili zisipandiane. Usiweke mafuta na acha nyama ziive taratibu huku ukiwa unageuza.

Geuza hadi nyama iwe rangi ya kahawia pande zote na kusiwe na damu wala maji. Hakikisha haiungui. Kama nyama haijaiva na inakauka, nyunyizia maji kiasi ili ipate kulainika vizuri na kuiva kabla ya kuila.

**Kuchanganya na mboga**

Nyama ikishaiva vizuri, weka mafuta ya kula vijiko viwili, acha yapate moto kiasi kisha weka kitunguu maji, koroga vizuri. Funika kiasi ili vitunguu vipate kulainika na kuiva vizuri na kuwa rangi ya kahawia.

Weka mboga mboga zilizobaki, kwa awamu. Koroga kila wakati kisha funika na mfuniko. Acha mboga iive kwa mvuke kwa dakika 5 hadi 7 na hakikisha haiungui.

Epua mboga, tenga pembeni na uandae chakula cha kujiramba.

# MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

## USIJENGE NYUMBA KWENYE UDONGO WA MFINYANZI



KUNA mambo mengi ambayo huchangia kuleta athari kwenye nyumba na hili tumekuwa tukijifunza kutoka katika maelezo ya watalaam mbalimbali kutoka kwenye sekta hiyo.

Watalaam hao wamekuwa wakisema kama ilivyo kwa vitu vingine kukumbana na changamoto mbalimbali, pia uchaguzi wa eneo la ujenzi wa nyumba linahitaji umakini mkubwa.

Miongoni mwa vitu ambavyo vimekuwa vikisisitizwa na wataalam hao ni pamoja na suala la kuzingatia au kuepuka kununua kiwanja na kujenga nyumba katika eneo ambalo linaweza kuleta athari kwenye nyumba yako baadaye.

Baadhi wamekuwa wakishauri kwamba japokuwa si utaratibu wa watu wengi, ni vyema na kwa usalama wa nyumba, kujenga utaratibu kabla ya kununua kiwanja kwa ajili ya matumizi ya ujenzi wa nyumba, ukawaona wataalam wakakushauri kama ni salama au laa.

Mtaalam wa shughuli za ujenzi, Victor Mkalama, anaeleza athari za kujenga nyumba kwenye kiwanja chenye udongo wa mfinyanzi kwamba udongo huo una tabia ya kuvimba na kuongezeka ukubwa hasa unapopata maji na pia unapokauka husinyaa.

"Kwa maana hiyo udongo unapovimba na kuongezeka ukubwa, jengo hunyanyuliwa juu, lakini udongo unaposinyaa jengo hutitia.

"Kuna aina nyingi za udongo wa mfinyanzi na katika kila aina ya udongo huo hutofautiana na aina nyingine katika kuvimba au kusinyaa na hii inasababishwa na kiasi cha unyevunyevu kwenye ardhi husika," anasema.

Kwa mujibu wa Mkalama, udongo wa mfinyanzi huvimba zaidi wakati miti iliyomo kwenye eneo husika linalotumika kujenga nyumba inapokatwa.

"Udongo hasa wa mfinyanzi huvimba zaidi wakati miti iliyomo inapokatwa, na hii inatokea kwa sababu mizizi hukomaa zaidi na kunyonya maji kwenye ardhi na kuchangia ongezeko la kiasi fulani cha unyevunyevu kwenye udongo huo," anasema Mkalama.

Anaongeza kwamba: "Kuondolewa kwa maji kwenye udongo wa aina hiyo ya mfinyanzi kwa kunyonywa na mizizi ya miti husababisha udongo kuongezeka au kupungua ujazo kwa kiasi fulani hususani katika kipindi cha kiangazi au masika.

"Na kuvimba au kusinyaa huko kwa udongo ni hatari kwa msingi wa nyumba kwa sababu huchangia kuleta nyufa kwenye nyumba na wakati mwingine kuiharibu kabisa."

# MPANGILIO

## DONDOO MUHIMU ZA KUWEKA SAMANI ZA KUHIFADHI VITU NDANI YA CHUMBA CHAKO CHA KULALA


1: Kama chumba chako kidogo hakikisha kitanda kinaambatana na droo ndogo pembeni yake kwa ajili ya kuhifadhi vitu vidogovidogo.

1: Weka meza ya kujiremba ambayo ina ndroo ambazo utahifadhia vitu kama vipodozi, mashine ya kunyolea nywele na vingine.

3: Weka meza ndogo ambayo unaweza kuweka glasi za za maji au kikombe cha kahawa.

4: Kama hauna meza ya kujeremba, weka kabati dogo ukutani nyuma ya kitanda ambalo litakuwa na uwezo wa kuhifadhi vitu vyako pamoja na nguo nyepesi.




KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
EBU NIAMBIE ULIKUWA UNABWABWAJA NINI PALE KIJIWENI WAKATI TUPO KWENYE MAPAMBANO!
MKE WANGU 'HII VAISI' ITA-NIONDOA HARAKA KULIKO 'UVIKO 19' AJASTI KIDOGO NIPATE UPEPO
KWA NINI HUTAKI NIKAOE KWETU?
MABINTI ZANGU NIKAWAOZE WAPI KAMA SIO KWENU NYIE WAPANGAJI?
JIRANI... MJINI HAKUNA CHOCHOTE! SISI HUKU NDIO TUNAFAIDI
KWELI TUNAFAIDI MAANA NIMEONA BARAKOA UNAVALISHA MIDOLI YA KUTISHIA NGEDERE SHAMBANI
USINIZINGUE... JIKOMITI NIKIKUKUTA NA MWANAMKE NIFANYE KITU...
HII NI TIKETI YA KUTAKA KUTEMBEA NA PETROLI NA KIBERITI
NDUGU MBONA HUINGIZI MKONO MFUKONI NAAGIZA MIMI TU?
MEZA MIDUME MITUPU LAZIMA MKONO UWE MZITO!
NIMEPOTEZA MATUMAINI YOTE!
USHAPEWA 'LOSI RIPOTI?'
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKISUBIRI KUKUBALIKA UTACHELEWA

## HABARI KIMATAIFA

# Wanajeshi wa Rwanda wawapa kipigo wanamgambo Msumbiji

**Maputo,** MSUMBIJI

WANAJESHI wa Rwanda walipelekwa nchini Msumbuji katika Jimbo la Cabo Delgado, wamefanya vizuri kwenye mapigano na wanamgambo, huku kukiwa na wasiwasi kuhusu kamanda wa kikosi hicho. Msemaji wa jeshi la Rwanda, Ronald Rwiyanga, aliiambia shirika la habari la Reuters, kwamba wanamgambo 14 wameuawa mapema wiki hii katika mapigano hayo.

Rwivanga alisema operesheni za kijeshi ziliendeshwa kwenye maeneo ya Mbau na Awese.

Alisema wanajeshi wa nchi hiyo walipata majeraha madogo na hali zao zinaendelea vizuri.

Mapema mwezi huu, Rwanda ilipeleka kikosi cha wanajeshi na polisi 1,000 nchini humo kusaidia katika kupamabana na kundi la waasi linaloendesha mashambulizi kaskazini mwa nchi hiyo.

Takriban raia laki nane walikimbia makazi yao kwenye mkoa wa Cabo Delgado, na kusababisha kampuni ya Mafuta ya Ufaransa ya Total kusitisha mradi wake wa gesi.

Kupelekwa kwa kikosi hicho cha Rwanda kulilenga kuwasaka wanamgambo wenye itikali kali na kuwadhibiti. Hata hivyo, wakosoaji wa serikali wanaoishi nchini humo wanaelezea hofu ya usalama wa wanajeshi wao.

**DW**



Kikosi cha wanajeshi wa Rwanda wakati kikiwasili nchini Msumbuji hivi karibu ni kukabiliana na wanamgambo wa IS. **(PICHAL DW)**

# Nchi 23 kukumbwa na baa la njaa

**NEWYORK,** MAREKANI

UMOJA wa Mataifa umeonya kuwa baa la njaa linatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 23 kwenye maeneo kadhaa duniani katika kipindi cha miezi mitatu inayokuja. Maeneo yanayokabiliwa na tishio hilo ni pamoja na mkoa wa Tigray nchini Ethiopia, kusini mwa Madagascar, Yemen, Sudan Kusini na kaskazini mwa Nigeria.

Mashirika mawili ya Umoja wa Mataifa, lile la chakula na kilimo (FAO) pamoja na mpango wa chakula duniani (WFP) yamesema katika ripoti yao mpya kwamba kati ya mwezi Agosti na Novemba hali ya ukosefu wa chakula itazidi kuwa mbaya kwenye maeneo hayo.

Kwa jumla ripoti hiyo imeyaorodhesha maeneo 23 duniani yaliyo kwenye kitisho kikubwa na mashirika hayo yametoa wito wa jumuiya ya kimataifa kujiandaa kutoa msaada utakaohitajika.

**DW.**

# ICC yamwachia huru mke wa rais

**THE HAGUE,** UHOLANZI

MKE wa Rais wa zamani wa Ivory Coast Simone Gbabgo, ameachiwa huru baada Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kumuona hana hatia dhidi ya mashtaka ya uhalifu wa kivita.

Simone alikamatwa na ICC na kukabiliwa na mashitaka ya uhalifu dhidi ya binadamu wakati wa mzozo wa kisiasa ulioukumba nchi hiyo kuanzia mwaka 2010 hadi 2011.

"Mahakama iliamua hati ya kukamatwa kwake imefutwa na haina umuhimu tena,"taarifa ya mahakama hiyo ilisema. Uamuzi huo wa kurasa saba wa Julai 19, mwaka huu, ulitolewa hadharani siku ya Alhamisi jioni.

"Habari njema kwa Bi Simone Gbagbo, sasa ataweza kusafiri akiwa uhuru kote ulimwenguni," alijibu wakili wake Ange Rodrigue Dadjé, katika taarifa yake.

Aliongeza "Kuondolewa kwa waranti huu kunakuja kumaliza kabisa kesi dhidi ya Simone Gbagbo mbele ya ICC,"

Simone Gbagbo alishtakiwa na ICC tangu 2012 kwa makosa manne ya uhalifu dhidi ya binadamu, ambayo ni mauaji, ubakaji, vitendo vingine visivyo vya kibinadamu na mateso, yaliyofanywa wakati wa mzozo huo.

Mgogoro huu, uliozuka kufuatia hatua ya aliyekuwa Rais Laurent Gbagbo, kukataa kutambua kushindwa kwake katika uchaguzi wa mwaka 2010, dhidi ya Alassane Ouattara, na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 3,000.

Mwezi Machi mwaka jana, ICC ilimuachilia huru Laurent Gbagbo, ambaye pia alishtakiwa kwa uhalifu dhidi ya binadamu, na aliweza kurudi nchini mwake.

**DW.**

## Irani yashutumiwa shambulio la meli

**TEL AVIV,** ISRAEL

IRANI imeshutumiwa kuwa nyumba ya shambulio dhidi ya meli ya mafuta katika pwani ya Oman, na kusababisha wafanyakazi wawili kuawa.

Hata hivyo, vyanzo kutoka Ulaya na Marekani vilisema ni mapema kuweka dhana hiyo kabla ya kupata vithibitisho katika tukio hilo.

Meli hiyo inayoitwa Mercer Street, inayotumiwa na kampuni ya Zodiac Maritime, yenye makao yake nchini Uingereza ni kampuni tanzu ya kampuni ya Zodiac inayomilikiwa na kampuni ya Eyal Ofer kutoka Israeli.

Tukio hilo lilitokea katika Bahari ya Arabia siku ya Alhamisi, kulingana na mmiliki wa meli hiyo, ambaye alitaja kama kitendo cha uharamia.

Wamiliki wa meli hiyo ambao ni raia wa Japan, walisema meli hiyo ilikuwa na bendera ya Liberia. Wafanyakazi wawili, mmoja kutoka Uingereza na mwengine kutoka Romania, waliuawa.

Afisa mmoja wa Israeli, aliyenukuliwa kwa sharti la kutotajwa jina na idhaa ya 13 ya Israeli, alikanusha kuwa kitendo hicho ni cha uharamia, akisema ni ugaidi kilichotekelezwa na Iran.

**RFI**

## Mbunge akamatwa kumkosoa rais

**TUNIS,** TUNISIA

VIKOSI vya Usalama nchini Tunisia, vimemkamata mbunge mmoja aliyelaani hatua ya Rais Kais Saied ya kusimamisha shughuli za bunge kwa siku 30.

Mbunge huyo Yassine Ayari, alitaja kitendo hicho kuwa sawa na mapinduzi ya kijeshi.

Chama chake cha HL kilisema Ayari alikamatwa na maofisa wa usalama wa Bunge ambao hawakutoa waranti wowote.

Hakuna uthibitisho wowote uliotolewa na Ikulu au ofisi ya mwendesha mashtaka, kuhusu kukamatwa kwa mbunge huyo.

Siku ya Jumapili iliyopita, Ayari, aliandika kupitia ukurasa wake wa Facebook kuwa hatua ya rais Saied ya kusimamisha shughuli za bunge na kumfuta kazi waziri mkuu ni mapinduzi.

Rais Saeid mwenyewe ametetea hatua hiyo kwa kusema ana nguvu chini ya katiba inayomruhusu mkuu wa nchi kuchukua hatua za dharura kunapotekea hali ya kitisho kwa taifa.

**DW.**

## SAFU

## MAKALA

# MAENDELEO BILA UMOJA NI UMASKINI



Na Magabilo Masambu

> **Tukiendelea kudhani na kukubali kwamba tuko wamoja wakati kuna kila dalili za kuonyesha kwamba tumeparaganyika, tutakuwa tunajaribu kutatua tatizo kwa tiba isiyo dawa.**

TANZANIA tuliongoza harakati nyingi za kiukombozi hasa katika nchi nyingi zilizoko kusini mwa frika. Umaarufu wetu ulitokana na umoja wetu katika kuhakikisha wale wote tuliowatangulia kupata uhuru nao wanakuwa huru angalau hata kwa uhuru wa bendera.

Kama wasemavyo waswahili umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, baada ya kupata uhuru mwaka 1961, kazi iliyokuwa imebaki ni kuijenga nchi. Ujenzi huu si wa siku moja na hautakuwa na kikomo kwa sababu matatizo yapo siku zote na hayatakoma.

Huko nyuma baada ya uhuru tulionekana kama tu wamoja kuliko tulivyo sasa. Kosa kubwa ambalo tutalifanya ni kutokubali kwamba sasa umoja wetu kama taifa hauko sawa. Tukiendelea kudhani na kukubali kwamba tuko wamoja wakati kuna kila dalili za kuonyesha kwamba tumeparaganyika, tutakuwa tunajaribu kutatua tatizo kwa tiba isiyo dawa.

Tumekuwa na mivutano pamoja na mabishano sana nchini. Si jambo baya kuvutana au kubishana maana inaonyesha uhai wa watu katika kufikiri kwa kupatia au kwa kukosea. Lakini mabishano yenye maana yanategemewa kuwa na mwisho mzuri wenye kutufanya tuwe wamoja zaidi kuliko kutugawanya.

Maendeleo hayatawezekana kama umoja wetu utakuwa na mashaka. Tunaweza kuwa kwenye safari moja lakini kila mmoja akawa na malengo yake na ikiwa hivyo ni jambo gumu kufikia mwisho wa safari yenyewe.

Tumekuwa taifa la majibizano badala ya mazungumzo. Hakuna wa kumlaumu, hakuna atakayetuambia tunakosea bali utashi wetu unaweza kupima matendo yetu na kugundua kwamba tunaendelea kukosea. Tunapokuwa na lugha gongana katika taifa, tunakuwa kama wajenzi wa mnara wa Babeli, ambao walishindwa kuendelea na ujenzi baada ya kutoelewana lugha.

Kama tunahitaji kujiletea maendeleo ya kweli, kwanza, tuna jukumu kama taifa kuhakikisha tunarekebisha tofauti zetu. Jambo hili litawezekana tu ikiwa tutajiona tuna haki sawa ya kushiriki kujenga nchi hii na kwamba hakuna kundi linalodhani kazi yake ni kuwaletea maendeleo wengine.

Tumekuwa na utamaduni wa kupendana, kusaidiana, kuoleana na kuheshimiana kama ndugu toka zamani. Sifa hii ndiyo iliyotutofautisha sisi na wao. Lakini naanza kuona kama tunazidisha juhudi za kufanana na wale tuliokuwa washauri wao. Kwa vyovyote vile watapenda tufanane na nyakati zao ili tusiwe na usemi tena mbele yao tuna kila sababu ya kukataa kwa vitendo siyo maneno tu.

Njia pekee itakayofanya kuwa wamoja ni majadiliano na hili si katika eneo la siasa tu ambalo linaonekana kwa urahisi kama tatizo mojawapo lenye kutufanya tusiwe wamoja, bali hata katika mambo mengine ambayo yanaleta mawazo mchanganyiko. Kuna wakati tunaweza kuwalaumu wale tunaotofautiana nao mawazo bila kufahamu kwamba tatizo liko kwetu.

Tunaweza kutofautiana katika baadhi ya mambo lakini yasitufanye tuvunje umoja wetu. Hofu, hisia na mazoea vinaweza kuwa sababu mojawapo katika kuvuruga umoja wa watu. Mipango ya maendeleo haitawezekana kama tunahofiana, tunachukiana, tunawindana, tunatuhumiana, tunadhulumiana na kadhalika.

Umoja tuliokuwa nao kama taifa ulijengwa juu ya misingi ya haki na usawa. Tunapoanza kuteleza katika misingi hiyo hatuwezi kutegemea matokeo tofauti na kutengana. Ili tuendeleze umoja huo ni muhimu kuheshimu misingi hiyo.

Tanzania kutokuwa na matatizo ya ukabila wala udini si kwa bahati mbaya bali ni kazi ilifanyika kuhakikisha kwamba mambo haya hayatugawi, tutaendelea na dini zetu au makabila yetu tukiwa wamoja. Kadhalika, mfumo wa vyama vingi vya siasa isiwe sababu ya kutugawa. Tunaweza kuwa na mfumo huu bila kugawanyika, tatizo moja naliona ni juu ya hofu kupata na kupoteza madaraka.

Tukubaliane kwamba kama nchi kuna wakati tunaweza kuwa tunapitia katika kipindi kigumu. Lakini ni busara zaidi katika kutazama changamoto mbalimbali zinazotufanya tusiwe wamoja. Tukizibaini tukae tuzungumze kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi badala ya kushtakiana. Bahati mbaya sana dunia ya leo imekuwa kama kijiji tofauti na awali ambapo jambo lolote lilifanyika bila dunia kuwa na habari.

Mwisho, kuna haja ya kuimarisha umoja na mshikamano wetu kama taifa. Tunaweza tusiseme lakini dhamiri zetu zinakiri juu hali halisi tuliyo nayo. Umoja wetu ndio maendeleo yetu, utengano wetu ndio umasikini wetu. Tunaweza kuchagua kuwa na maendeleo au tuendelee kuwindana tuwe maskini zaidi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA- TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Jafongo' malori ya mkaa yaliyotisha watoto



Na Adam Fungamwango

KWA sasa serikali inapiga vita sana kukata miti, hivyo biashara ya mkaa si maarufu kama ilivyokuwa zamani. Kwenye miaka ya 1970 hadi katikati ya 1990, karibu kila mtaa kwenye mikoa mbalimbali nchini Tanzania hasa Dar es Salaam na Pwani kulikuwa na stoo za mkaa.

Wananchi wengi wakati huo walikuwa wakitumia kwa kupikia. Kwa sasa angalau watu wameendelea kidogo, ingawa bado ipo lakini si kama ilivyokuwa zamani.

Hivi sasa watu wanatumia majiko ya umeme, gesi, majiko ya China na mengine wanayofanana na hayo. Enzi hizo hata mtu anayetumia mkaa hata yeye anaonekana kidogo hajambo kwa sababu wako waliokuwa wakitumia kuni, vifuu vya nazi na vitu vingine ambavyo vitaonekana vinaweza kuhifandhi moto kwa ajili ya kupikia.

Japo bado kuna baadhi ya watu wanatumia kuni na vifuu, lakini kwa sasa itakuwa ni vijijini zaidi. Lakini enzi hizo hata Dar es Salaam tu watu walikuwa wakitumia kuni. Kwa sasa zinatumika zaidi kwenye shuguli za kijamii kama misiba na sherehe.

Wakati miji mikubwa ikiwa na stoo za mkaa, malori yaliyokuwa wakitumika kupeleka mkaa huo kutoka shamba mengi yalikuwa ni aina ya 'Jiefang'. Haya ni aina ya magari 'magumu' ya Kichina yaliyotengenezwa miaka ya 1950 kwa msaada wa Jeshi la Kisovieti. Malori hayo yalitengenezwa na kiwanda cha First Automobile Works na kupewa jina la 'FAW Jiefang.'

Kwa wale waliowahi kuangalia filamu za Kimarekani, hasa zile za vita nchini Vietman, sasa yale malori ambayo Wavietnam wanapanda kupigana vita na wamarekani, asilimia kubwa ni 'Majafongo'.

Nchini Tanzania, kwenye miaka ya 1970, baadhi yalikuwa jeshini lakini mwishoni mwa miaka hiyo na mwanzoni mwa miaka ya 1980, hata raia walianza kuwa nayo na kazi kubwa ilionekana ni kufuata mkaa porini.

Nadhani ilikuwa hivyo kwa sababu yalikuwa ni magari imara 'chuma cha pua' yaliyokuwa na uwezo wa kwenda na kuingia sehemu yoyote. Yalikuwa na uwezo wa kupita kwenye barabara ya aina yoyote, hata ikiwa mbovu kiasi gani. Haikuangalia majira, iwe mvua au jua, 'Jafongo' liliweza kupita bila matatizo yoyote yale.

Ndiyo maana ilikuwa huwezi kukuta eti 'Jafongo' limekwama porini lilipokuwa likienda kuchukua mkaa.

Hata mijini wakati huo, bado barabara hazikuwa nzuri kihivyo. 'Jafongo' lilikuwa na uwezo na kupita kwenye barabara mbovu za mitaani pamoja na ukubwa wake wote huku likiwa na shehena ya magunia ya mkaa bila matatizo. Ukiliona limesimama basi ujue limeharibika lintengenezwa, lakini siyo kukwama kwa ajili ya barabara za michanga, matope, miinuko na mabonde, wala njia zenye mashimo.

Muundo wa malori hayo ndiyo balaa. Kwanza kabisa ni kwamba ina sehemu ya kuiwasha mbele. Kuna sehemu mbele ya bodi, lori hilo linaweza kuwashwa mtu akiwa nje ya gari kwa kutumia 'handle'.

Zina mwonekano wa kutisha mno kwa mbele na hasa watoto kuanzia miaka miwili, hadi saba hivi, walikuwa yakiyaogopa mno pindi tu wanapoyaona.

Wazazi waliwatishia watoto kuwa watawapeleka kwenye 'Jafongo' pale wanapoona wanakataa kutumwa, kula au kufanya kitu chochote kinyume cha maadili na watoto walinyooka kwa jinsi walifahamu lori hilo.

Acha sura yake ya mbele inavyotisha, mungurumo wake wa kukera ndiyo kabisa inalifanya kuwa moja ya magari yaliyokuwa yanatisha sana kwa mwonekano, ukiachilia mbali lori aina ya FIAT.

Madereva wa malori hayo wakati huo ni lazima wawe wameshiba. Nina maana lazima awe na nguvu kwa sababu usukani wake ni mpana mno na mgumu si kama malori haya ya sasa.Vinginevyo, dereva tu hivi hivi hata kona inaweza kukushinda kukata.

Huwezi kumkuta dereva wa 'Jafongo' wakati huo akiwa msafi. Kwanza kutokana na ukweli kwamba anaendesha gari ambalo kwa zaidi ya asilimia 90 yalikuwa ya kubeba mkaa lakini pia ni lazima awe fundi pia kwa sababu likiharibika basi awe na uwezo wa kutengeneza.

Kumbuka mpaka yakiwa yamefikia kumilikiwa na watu binafsi, basi walikuwa yamepita sehemu nyingi, hivyo tayari yalikuwa yameshakuwa makuukuu, licha ya kwanza bodi zake zilikuwa ziko vile vile 'chuma cha pua'.

Pamoja na breki zake za kawaida, lakini utingo wa 'Jafongo' alikuwa lazima awe na mti mkubwa hivi, mfano ya gogo dogo. Kazi yake gari ikisimama ni kwenda kuweka gogo mbele ikifanya kazi ya 'hand break'.

Wakati watoto wadogo walikuwa wakiliogopa, wavulana kuanzia miaka 12, hadi 15, wao walikuwa na kazi moja tu ya kuwatania utingo wa malori hayo ya mkaa na wabebaji, na ilikuwa vita kubwa maneno kati ya wavulana wa wakati huo na utingo wao.

Walikuwa wakiwatania kutokana na kuwa weusi uliotokana na masizi ya mkaa, kwani kutwa nzima kazi yao ilikuwa kusambaza mkaa kwenye stoo, hivyo nguo zao na jinsi walivyo, kwa wavulana ambao wakati huo ndio walikuwa wanaanza kupata akili na bado haijakomaa, kwao ilikuwa burudani kuwaona na kuwatania.

Hayo ndiyo malori aina ya 'Jafongo' yaliyokuwa na mwonekano wa kutisha, yaliyotesa sana miaka hiyo. Hata ukitaka kugombana na mtu we mwambie tu. 'sura kama Jafongo'. Ugomvi wake hautoisha mapema.

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald kijana msomi aliyetoka nchini Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya mapenzi-17

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HAKUJUA hatima ya baadaye. Ni kwamba amrejee Doroth au afanye nini. Tausi ameshafariki.

Hili kwanza alilicha kiporo. Bado alikuwa na mambo mengi yaliyokuwa yanamtatiza akilini.

Aliwaza mengi. Alichokuwa akiwaza ni jinsi kifo cha mpenzi wake kilivyotokea.

Ni jana tu, Kamanda wa Polisi Kanda ya Kinondoni akitoa taarifa ya daktari juu ya kifo cha msichana huyo ambapo ilisemekana pamoja na kudaiwa kurushwa kutoka kwenye bodaboda au gari, lakini pia iligundulika kuwa alipigwa risasi kichwani.

"Ina maana Tausi aliuawa. Nani alimuua?" Alijiuliza. Baadaye alikumbuka maongezi yake na Sadiki, kabla ya kwenda Magomeni Makuti baada ya kutoonekana kwa siku tatu.

"Mimi mwenyewe na ndugu zake tumetafuta kila sehemu wapi. Kona zote tumezunguka. Hospitali mbalimbali. Nimekupigia sana simu rafiki yangu kwa namba zako zote mbili, siku ya tatu hii hupatikani. Nilivyoona hivyo akili ikanijia kuwa labda uko naye, kwa sababu nakumbuka siku alipoondoka alisema unamwita ili mkutane."

"Nilimwita tukutane?" Alijiuliza. Anachokumbuka hakumwita.

"Je, alimdanganya Sadiki kuwa yeye anamwita, lakini aliitwa na mtu mwingine?"

Alitaka kujua kila kitu kilichotokea. Alitaka kujua ni nani alimwita. Kwa nini alikwenda Sinza na kwa sababu gani aliuawa, kwani pamoja na ajali ya bodaboda kama baadhi ya mashuhuda walivyosema, lakini polisi waligundua risasi iliyokwama kichwani.

Akiwa kwenye hali ya mawazo mlango uligongwa. "Fungua uko wazi." Alijibu.

Aliyeingia ni Doroth. Aliingia taratibu sana na kwenda kukaa kwenye kiti kidogo pembeni ya kitanda.

"Hujambo?" Alisalimu.

"Sijambo." Donald aliitikia kwa sauti ya chini kama vile hakuipenda salamu hiyo.

"Vipi unaumwa?"

"Hapana siumwi, ila najisikia vibaya."

"Pole."

"Ahsante."

"Lakini kujisikia vibaya ndiyo hata kazini hujaenda siku ya nne sasa?"




**"Mpenzi nimemtuma kijana mmoja wa bodaboda aje kukuchukua. Ni rafiki yangu na huwa namlipa kwa mwezi kwa ya mambo ya dharura. Nimekwita ghafla ndiyo maana sitaki uingia gharama, atakuleta salama hadi huku."**

"Wewe nani kakwambia kama siku nne sasa sijaenda kazini?" Donald naye aliuliza. "Basi tuyaache." Doroth alimhisi.

Baada ya maongezi ya dakika 20 hivi, Doroth aliaga kuwa anakwenda dukani kwake. Doroth aliona bado Donald hayupo kwenye hali yake ya kawaida. Akajipa matumaini kuwa atakapoanza kumsahau Tausi, penzi litarudi kwake.

Mtu mwingine aligonga hodi. "Karibu." Aliyeingia sasa ni mdogo wake wa mwisho Fau mwenye miaka 12. Aliingia akiwa na chakula. 'Kaka chakula hiki."

"Ahsante. Niletee na simu yangu hapo kwenye chaji."

"He, kaka simu hii si nilimuona nayo mama siku ile anampa baba aweke kwenye droo?"

"Lini?"

"Siku ile ambayo wewe ulikuwa unalalamika simu yako imeibwa."

Donald akapatwa na mshtuko.

"Kweli?" "Kweli tena kaka, ndiyo hii hii." "Sasa Fau, mimi nilikuwa natafuta simu imepotea kwa nini usiniambie?"

"Mimi sikujua. Mimi nilijua ya mama anampa baba amuwekee. Kwani nilijua kama yako? Ningejua si nigekwambia kuwa simu anayo mama."

"Ina maana mama ndiyo aliichukua?"

"Sijui, lakini mimi nilimuona nayo anampa baba, halafu baba akaiweka kwenye droo."

Kengele ya hatari ikaanza kulia kwenye kichwa cha Donald.

Akaanza kuhisi kuwa huenda simu yake haikupotea kwa bahati mbaya. Ilichukuliwa. Hata kupatikana kwake ilipatikana kiutata. Ilipatikana sehemu ambayo alipita mara kadhaa kuitafuta, lakini hakuiona. Cha ajabu kesho yake akaiona. Akadhani kuwa huenda alikuwa anaipita haioni.

"Basi Fau, usimuambie yeyote hili tuliloongea hapa unasikia? Usimwambie baba wala mama." Fau aliitikia kwa kichwa.

"Halafu kuna kazi moja nitakutuma uifanye, halafu nitakupa zawadi nzuri, sawa?"

"Ndiyo kaka." Aliitikia.

Swali likawa moja alilojiuliza "Ni kwa nini simu yake ilichukuliwa?"

****************************

Hakuamini alichokuwa akikisoma. Kwa haraka alitoa meseji zote ambazo alikuwa na wasiwasi nazo na kuzihamishia kwenye simu yake.

Alimwita tena Fau na kumwambia airudishe simu ya baba yake pale pale ilipokuwa kwenye chaji, akimsihi kutomwambia mtu yoyote yule.

Sasa alitaka kuwa na uhakika na kile achokuwa akikisoma. Alikwenda kujilaza kitandani. Akachukua simu yake na kuzifungua tena zile meseji ambazo zilitoka kwenye simu ya baba yake mzee Peterson.

Alichofanya Donald ni kumwambia mdogo wake Fau kuivizia simu ya baba yake siku akichaji, aichukue na kumletea.

Ilikuwa ni siku ya tatu, mzee Peterson alipochaji simu yake chumbani na yeye mwenyewe kwenda kulala kabla ya kupitiwa na usingizi mzito. Ilimpa nafasi Fau na kuichukua, akaipeleka kwa kaka yake.

Pamoja na kwamba meseji zilifutwa, lakini Donald alikuwa ni mtaalam kidogo ya mambo ya simu za mkononi. Wengi hufuta meseji kwenye simu, lakini kuna sehemu ambazo zinakuwepo na kama si mtaalam huwezi kubaini hilo.

Donald alizikuta meseji nyingi, lakini alizichukua zile tu ambazo alikuwa ana wasiwasi nazo na simu ikarudishwa. Alianza kusoma meseji ya kwanza.

"Samahani mpenzi, nimepoteza simu yangu muda si mrefu, ndiyo maana nimetumia namba ambayo ni ngeni nimeomba kwa rafiki yangu, nakuomba uje hapa Afrika Sana, niko hapa nakusubiri."

Akaendelea kusoma ya pili

"Mpenzi nimemtuma kijana mmoja wa bodaboda aje kukuchukua. Ni rafiki yangu na huwa namlipa kwa mwezi kwa ya mambo ya dharura. Nimekwita ghafla ndiyo maana sitaki uingia gharama, atakuleta salama hadi huku." Akaelekea kwenye meseji ya tatu.

"Amevaa sketi fupi yenye mistari myeupe na myeusi kama ya pundamilia hivi na blauzi nyeupe."

Alipoangalia meseji zote zilitumwa siku ambayo yeye alikuwa amepoteza simu yake kimaajabu.

Aligundua pia meseji zile zilitumwa kuelekea kwenye namba ya marehemu mpenzi wake Tausi.

Alichogundua ni kwamba wizi wa simu yake ulifanya kwa makusudi ili apoteze mawasiliano na mpenzi wake kwa ajili ya wao kuwasiliana naye kwa nia ya kumdanganya.

**INAENDELEA JUMAPILI**

# BURUDANI



## LINEX SASA UNATAFUTA UBAYA



MWANAMUZIKI wa siku nyingi, Linex Sunday, amesema ladha ya muziki wa Bongofleva imeshuka na kuomba Mungu aunusu kwa kuupa mwisho mzuri.

Linex amesema endapo mtu akisema kweli kuhusu muziki anaonekana ana chuki ila binafsi yake haoni kitu kwa sasa.

"Mziki wetu wa Tanzania ukiuzungumzia kwa asilimia 100 utaonekana una chuki, lakini sioni daah' Mungu awape uamsho waimbaji wote," amesema.

## P Mawenge akumbuka alivyoachwa



RAPA P Mawenge, amekumbuka jinsi alivyoachwa na mpenzi wake baada ya kutumiwa picha na shabiki wake wa kike.

P Mawenge amesema kitendo hicho kilimfanya kuachwa na mpenzi wake huyo ambaye alidumu naye kwa kipindi cha miaka minne.

"Kuna mwanamke alinitumia picha za WhatsApp, sasa mpenzi wangu akaona picha zile za ajabu ajabu zinaingia ilinileteа matatizo sana, ni mtu ambaye tulikuwa tumezoeana " amesema

Aidha msanii huyo ameongeza "Niliachika kwa sababu ya drama unajua ulimwengu wa sasa hivi una sababu nyingi sana za watu kugombana kwenye uhusiano,"

# BEN POL ARUDI AKILALAMIKIA MAHABA

MKONGWE katika muziki wa RNB, Ben Pol amerudi tena katika anga la muziki baada ya kukaa kimya kwa muda mrefu.

Hata hivyo, ujio wake unaonekana kutawaliwa na machungu mengi ya mapenzi kiasi ambacho katika nyimbo zake nne zinazokuja zinazungumzia shubiri katika uhusiano aliopitia na wanawake kadhaa.

Kazi hizo kwa pamoja ameziita kwa jina la 'B' zinajumuisha nyimbo ya Kisebusebu ambao amemshirikisha Billnass.

Pia kuna nyimbo nyingine kama "For you, Unaita na Warira ambazo zimetayarishwa na Chatta Vintage, Jaco Beatz na O Righty.

## HABARI MICHEZO




# ANCELOTTI

## AMTAKA RICHARLISON MADRID

**MADRID,** Hispania

KOCHA Carlo Ancelotti amesisitiza Real Madrid wanahitaji kumsajili mshambuliaji kwa ajili ya msimu unaokuja, huku akimtaja Richarlison anafaa katika nafasi hiyo, kwa mujibu wa El Confidencial.

Real Madrid wanakosa mabao mengi kutokana na safu yake ya ushambuliaji kutokuwa na makali sana na kocha huyo raia wa Italia anataka kurekebisha hilo katika soko hili la uhamisho wa wachezaji.

Ripoti hiyo inadai Ancelotti anamwona Richarlison kama chaguo bora la kuimarisha nafasi hiyo, haswa kutokana na tatizo la kifedha katika kumpata Erling Haaland au Kylian Mbappe.

Raia huyo wa Brazil ambaye yuko kwenye Michezo ya Olimpiki, alimnoa wakati akiwa anaifundisha Everton.

Richarlison anaweza kucheza pembeni, anajua kupiga mashuti nje ya sanduku na ana kiwango kizuri.

Na kwa sababu hiyo Ancelotti anamwona anaweza kuwa msaidizi mzuri zaidi kwa Karim Benzema.

Richarlison mwenye umri wa miaka 24, amekuwa Everton kwa misimu mitatu, akiwa amewasili hapo mwaka 2018 akitokea Watford.

Amefunga mabao mabao 14, 15 na 15 katika misimu yake mitatu akiwa hapo Everton.



## MILAN YAWANIA SAINI YA ZIYECH

**MILAN,** Italia

KLABU ya AC Milan imeweka wazi mipango ya kutaka kumsajili kiungo mshambuliaji wa Chelsea, Hakim Ziyech raia wa Morocco katika majira haya ya kipindi cha joto.

Kwa mujibu wa Calcio Mercato, Milan wanamtaka kwa mkopo wenye chaguo la kumnunua moja kwa moja, huku Chelsea wakisisitiza watakuwa tayari kumuuza moja kwa moja na sio kumtoa kwa mkopo.

Chelsea wamekuwa na uhusiano mzuri na Milan hasa baada ya kufanya biashara na wachezaji wawili wa klabu hiyo, Fikayo Tomori na Oliver Giroud katika msimu huu.

Chelsea walimnunua Ziyech kutoka Ajax msimu uliopita kwa dau la euro milioni 40, tangu ajiunge na timu hiyo amefanikiwa kufunga mabao sita na kutengeneza mengine manne katika mechi 39 alizocheza katika mshindano yote.

Na inaonekana wazi hayupo kwenye mipango ya Kocha, Thomas Tuchel ambaye hakumpa nafasi ya kutosha msimu uliopita.

# ZOUMA AKATAA KUTOLEWA CHAMBO

**LONDON,** England

MPANGO wa Chelsea kumsajili, Jules Kounde kutoka Sevilla ya Hispania umeingia utata baada ya kuibuka ripoti kwamba beki, Kurt Zouma anasita kuwa chambo.

Zouma anatakiwa kujiunga na Sevilla kama sehemu ya dili la pauni milioni 50 ili Kounde aweze kutua hapo kwenye viunga vya Stamford Bridge.

Mkurugenzi wa Chelsea, Marina Granovskaia na Mkurugenzi wa Soka wa Sevilla, Ramon Rodriguez Verdejo'Monchi'wamekuwa na mazungumzo zaidi kukamilisha dili la Kounde.

Hata hivyo, Beki wa Chelsea Zouma anafikiria kwa kina kukataa kutumika kama mpango wa kubadilishana katika juhudi za kumsajili Kounde hali itakayokuwa kikwazo kikubwa.

Beki huyo wa kati wa Chelsea, Zouma anataka kubaki Ligi Kuu England hasa pale London kabla ya msimu mpya kuanza.

Ripoti zimesema West Ham imeweka nia ya kumsajili Zouma na iko katika majadiliano kuhusu uhamisho wenye thamani ya pauni milioni 20.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LIVERPOOL YAHITAJI KUMSAJILI LOCATELLI

Ni kwa ajili ya kuziba pengo lililoachwa na Wijnaldum ambaye amejiunga...

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imeingia kwenye mbio moja na Juventus na Arsenal kuwania saini ya mchezaji wa kimataifa wa Italia, Manuel Locatelli, 90min imeripoti.

Locatelli alionyesha kiwango cha kuvutia zaidi kwenye michuano ya Euro 2020, wakati Italia ikitwaa taji hilo kwa kuifunga England katika mchezo wa fainali.

Nyota huyo Locatelli alifunga mabao mawili kwenye mchezo dhidi ya Uswisi na hivyo kuzivutia klabu kadhaa kubwa Ulaya.

Kiungo huyo wa zamani wa AC Milan, alijiimarisha yeye mwenyewe kule Sassuolo alikocheza kwa misimu miwili kwenye Serie A na sasa huduma yake imekuwa lulu barani Ulaya.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Liverpool wanatarajia kutoa ofa rasmi kwa klabu yake ya Sassuolo ili kumvuta pale kweye viunga vya dimba la Anfield.

Liverpool wanatafuta mchezaji wa kuziba pengo la Georginio Wijnaldum ambaye aliondoka kama mchezaji huru na kujiunga na miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, Paris Saint-Germain.

Awali Arsenal ilishaweka mezani ofa ya pauni milioni 37, ambazo zilionekana kutokubaliwa na Sassuolo.

Juventus nayo ikatupa karata yake na sasa wapo kwenye hatua za mwisho kutuma ofa yao kwa ajili ya kunasa saini ya mchezaji huyo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti hiyo, Juventus wana nafasi kubwa zaidi ya kumsajili nyota huyo kwa sababu ameonyesha nia ya kwenda kucheza kwa kibibi kizee hicho cha Turin.

## KWA UFUPI

### MADRID, PSG KUTETA

REAL Madrid itafungua mazungumzo na Paris St-Germain katika wiki zinazokuja ili kumsajili straika wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, huku mkataba wake wa sasa ukiwa unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja. (90min)

### GREALISH KUNEEMEKA

ASTON Villa wamempa ofa ya mkataba mpya, kiungo Jack Grealish mweye umri wa miaka 25, ambao utamfanya alipwe mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki, ikiwa ni sehemu ya kumshawishi asiende Manchester City, ambao wameweka ofa ya pauni milioni 100 ili kumsajili. (Star)

### POGBA AWEKA NGUMU

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, ambaye amekuwa akihusishwa sana na uhamisho wa kwenda Paris St-Germain, hatasaini mkataba mpya na mashetani wekundu hao. (Sky Sports)

### PSG KIMYA KIMYA

KOCHA wa PSG, Mauricio Pochettino amesema klabu "inafanya kazi kwa ukimya" kwenye kipindi hiki cha usajili wa wachezaji. (Le Parisien, via Metro)

### SPURS YAMTAKA ROMERO

TOTTENHAM Hotspur imetoa ofa kwa Atalanta ya pauni milioni 43 kwa ajili ya kumsajili mlinzi wa Argentina, Cristian Romero mwenye umri wa miaka 23. (Sky Sports Italia, via Mail)

### JAMES NJIA PANDA

KIUNGO wa Colombia, James Rodriguez, amesema hana uhakika kama atabaki Everton, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 ameondoa uwezekano wa yeye kurudi Real Madrid. (Mail)

### KLOPP AMTAKA NEUHAUS

KIUNGO wa Borussia Monchengladbach na Ujerumani, Florian Neuhaus mwenye umri wa miaka 24, anawaniwa na Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp. (Sport1)

### VILLA YAWEKA MGOMO

KLABU ya Southampton imekataa ofa ya pauni milioni 25 kutoka Aston Villa kwa ajili ya kumsajili kiungo wake, James Ward-Prowse mwenye umri wa miaka 26. (Athletic)

### BRUCE MAMBO SAFI

KOCHA wa Newcastle United, Steve Bruce anatarajiwa kupewa ofa ya mkataba mpya wa miaka mitatu. (Star)

### ABRAHAM SOKONI

CHELSEA inajiandaa kupunguza bei yao ya pauni milioni 40 ya kumuuza straika wake mwenye umri wa miaka, 23 Tammy Abraham, ambaye amezivutia pia Arsenal, West Ham na Aston Villa. (Sun)

### XHAKA KITAELEWEKA

ARSENAL inajiandaa kumpa ofa ya mkataba mpya kiungo wake, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 28. (Athletic)

HABARI MICHEZO

# KARIA AMKABIDHI SAMIA KOMBE LA CECAFA U-23

**Na Adam Fungamwango**

RAIS wa Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Wallace Karia, amesema ubingwa ambao Tanzania umepata katika mashindano ya vijana ya umri chini ya miaka 23, ni zawadi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Samia Suluhu Hassan.

Tanzania ilitwaa ubingwa wa michuano hiyo baada ya kuwafunga yosso wenzao wa Burundi penalti 6-5.

Akizungumza baada ya Tanzania kutwaa ubingwa huo, Karia ambaye pia ni Rais wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), alisema kikosi chake kilipambana kupata kombe hilo na kutoa zawadi kwa kiongozi huyo kupokea ushindi huo baada ya mapema kupokea ndege.

"Kwanza kabisa tuliongea na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akatuambia Rais (Samia), amepokea ndege, sasa anatakiwa apokee pia na zawadi ya kombe, na kweli sisi na vijana wetu tumetekeleza hilo, tunampelekea mama zawadi ya kombe," alisema Karia.

Hata hivyo alisema kuwa haikuwa kazi rahisi kutwaa ubingwa huo kutokana na maandalizi finyu waliyofanya huku mechi zote walizocheza kuwa na ushindani mkubwa.

"Hatukuwa na maandalizi mazuri. Mwalimu alikuwa na wasiwasi kwa sababu wachezaji walikusanyika mara baada ya Ligi Kuu kumalizika. Wengine walishindwa kuja kwa sababu walikuwa wanamalizia mechi ya Simba na Yanga. Wengine walibaki kwa sababu ya kucheza mechi za mchujo." alisema Karia.

Aliongeza awali ilikuwa ichezwe michuano ya Kombe la Chalenji, lakini yeye kama Rais wa CECAFA akawashawishi wenzake ichezwe ya vijana ili kuwapa uzoefu na kutengeneza timu za taifa za baadaye kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Karia pia amewaomba Watanzania kujitokeza viwanjani kuhudhuria michuano ya Kombe la Kagame ambayo inatarajiwa kuanza leo hapa nchini.

"Niwaambie Watanzania, tumepata bahati, waje kwa wingi viwanjani. Tumejiandaa vizuri. Tunaomba tuzipe moyo timu zetu tatu, KMKM, Yanga na Azam ili mojawapo ichukue kombe. Ninawaambia Watanzania tuache mambo ambayo hayana maana. Twende kwenye mambo ambayo yanajenga, "alisema Karia.

Yanga inatarajia kuanza kuwania ubingwa wa michuano hiyo kwa kuwakaribisha Nyasa Big Bullet ya Malawi kuanzia saa 10:00 jioni leo wakati mapema mchana Express kutoka Uganda itavaa na Atlabala ya Sudan Kusini huku kesho Azam ikishuka dimbani kuwakabili KCCA ya Uganda.




Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Wallace Karia (kulia), akiwa amebeba kombe la ubingwa wa mashindano ya vijana wa umri chini ya miaka 23 (U-23), ya Afrika Mashariki na Kati baada ya Tanzania kutwaa taji hilo juzi katika Mji wa Bahir Dar, Ethiopia. Kushoto ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa TFF, Athumani Nyamlani. **PICHA: MTANDAO**.

# Golikipa Mrundi akaribia Yanga

**Na Saada Akida**

GOLIKIPA Eric Johora kutoka Aigle Noir ya Burundi, amesema yuko kwenye mazungumzo na uongozi wa Yanga kwa ajili ya kusaini mkataba wa kutumikia timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa.

Kwa sasa Johora ni mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba na timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya Burundi na anatarajiwa kuidakia Yanga katika mashindano ya Kombe la Kagame yanayofanyika kuanzia leo hapa nchini.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Johora alisema mazungumzo yake na Yanga yako katika hatua nzuri na wakati wowote atasaini mkataba wa kuwatumikia.

Johora alisema kabla ya kutua nchini, alipata ofa kutoka katika klabu mbalimbali na ndio sababu alikataa kusaini mkataba mwingine na Aigle Noir ambayo mwaka jana ilicheza mchezo wa kirafiki na Yanga.

"Niko nchini kuzungumza na Yanga, bado sijasaini mkataba kwa sababu mazungumzo yanaendelea, kuna mambo tunayaweka sawa na yakikamilika muda wowote nitasaini mkataba na Yanga," alisema mlinda mlango huyo.

Alisema anaamini kiwango chake na endapo watakamilisha mazungumzo na kutua Yanga, basi mashabiki wa timu hiyo wajiandae kuona mambo mazuri kutoka kwake kutokana na uzoefu aliokuwa nao.

Ujio wa golikipa huyo ni ishara kwamba Metacha Mnata na Farouk Shikalo wamekalia kuti kavu lakini uamuzi wa kusajiliwa kwa Johora utajulikana kufuatia kiwango atakachokionyesha kwenye mashindano ya Kombe la Kagame.

## Mbeya Kwanza FC kutohamia Kigoma

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mbeya Kwanza umesema hawana mpango wa kuihamisha timu hiyo katika Mkoa wa Kigoma na sasa imeanza maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kauli hiyo imetolewa baada ya kuwapo na tetesi kuwa timu hiyo iliyopanda daraja pamoja na Geita Gold FC iko kwenye mchakato wa kuhamishiwa Kigoma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Mbeya Kwanza, Mohammed Mashango, alisema hakuna mpango wa kubadilisha jina wala makazi ya klabu hiyo na kusisitiza itabakia katika jiji la Mbeya.

Mashango alisema kwa sasa wanapambana kufanya usajili na kuangalia wachezaji wazuri kutoka ndani na nje nchi ili kuimarisha kikosi chao kwa ajili ya kujipanga kukabiliana na ushindani.

"Tutaendelea kubaki Mbeya na ndio tutatumia uwanja wa nyumbani, tayari tumeshaanza usajili kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi kwa sababu hatutaki kushiriki kwa msimu mmoja na baada hayo tunarudi chini, tumejipanga vizuri, tumeangalia wachezaji wa ndani na nje ikiwamo Zambia na Burundi," alisema Mashango.

Aliongeza hawana mpango wa kubadilisha benchi la ufundi kwa sasa na wameamua benchi lao la ufundi litaendelea kuwa chini ya Kocha Mkuu, Matata Hussein ambaye ndiye aliipandisha timu hiyo.

## Temeke Jogging wapata viongozi

**Na Mwandishi Wetu**

RASHIDI Mvogogo ameibuka mshindi katika nafasi ya Mwenyekiti kwenye uchaguzi wa Chama cha Mbio za Polepole cha Wilaya ya Temeke (TEJA), ambacho kilifanya uchaguzi wake kwenye Ukumbi wa Manispaa ya Temeke jijini Dar es Salaam juzi.

Akitangaza matokeo ya uchaguzi, Mwenyekiti wa Kamati ya Muda, Ramadhan Namkoveka alisema Mvogogo aliibuka kidedea baada ya kupata kura 75 dhidi ya Mussa Mtulia aliyeambulia kura 52.

Namkoveka alisema nafasi ya Makamu Mwenyekiti ilikwenda kwa Janeth Maseke aliyepata kura 116, huku aliyeshinda cheo cha Katibu Mkuu ni Njoku Hasan Yasin ambaye alipata kura 108 na nafasi ya Katibu Msaidizi ilikwenda kwa Saweli Kiogolo aliyepata kura 113.

Juma Ahmad Juma aliyepata kura 116 alichaguliwa kuwa Mweka Hazina, wawakilishi wa wanawake waliochaguliwa ni Fatma Mayele kura 120 na Anna Peter kura 117. wakati Wajumbe waliopatikana ni Ramadhan Kitunguu, Iddi Mbelwa, Mshauri Omar, Hussein Ngulungu, Sande Kichumvi, Shaaban Shaibu, Ebrahim Daffi na Kumbuka Sozigwa.

Uchaguzi huo umefanyika kwa kushirikisha wajumbe 130 kutoka katika klabu 44 za jogging za wilaya hiyo na umefanyika baada ya kukamilika kwa mchakato wa marekebisho ya Katiba uliofanyika Juni 6, mwaka huu

Michezo
Jumapili Agosti 1, 2021
Nipashe



Liverpool yahitaji kumsajili Locatelli

HABARI UK 22

## Kakolanya azidi kujipanga Simba

Na Saada Akida

KUELEKEA msimu mpya wa 2021/22, golikipa, Beno Kakolanya amesema ataendelea kupambana kuhakikisha anapata nafasi ya kucheza katika kikosi cha kwanza cha mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam na kamwe hatakata tamaa.

Kakolanya alisaini mkataba mpya wa miaka miwili na Simba, siku chache baada ya kikosi hicho kurejea nchini kikitokea Afrika Kusini kuwakabili Kaizer Chiefs kwenye mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hata hivyo, kuna tetesi Wekundu hao wa Msimbazi tayari wameshakamilisha mazungumzo na golikipa wa Tanzania Prisons, Jeremiah Kisubi.

Kakolanya aliliambia gazeti hili ataendelea kujiimarisha ili kulinda nafasi yake ya chaguo la pili kwenye kikosi hicho ambacho, Aishi Manula ndio golikipa namba moja.

"Mimi bado nipo sana Simba, nilisaini mkataba mpya na nitapambana ili kufikia malengo yangu, kikubwa nitahakikisha nailinda nafasi yangu ya kuwa kipa chaguo la pili," alisema Kakolanya.

Katika kuhakikisha Simba inafanya vizuri zaidi katika msimu ujao, imepanga kukifanyia maboresho machache kikosi chake na hatimaye kuendelea kupeperusha vyema bendera ya klabu yake.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema lengo la kumsajili Kisubi ni kuendelea kumpa changamoto ya kujiimarisha, Manula ambaye pia ni Tanzania One.

Nyota wengine wanaodaiwa kusajiliwa na Simba ni pamoja na straika wa Mbeya City, Kibu Dennis na beki wa kulia wa KMC, Israel Mwenda ambaye amekiongoza vyema kikosi cha Tanzania (U-23), kutwaa ubingwa wa CECAFA huko Ethiopia.



Golikipa wa Timu ya Soka ya Tanzania ya vijana wa umri chini ya miaka 23, Metacha Mnata, akiwa na kombe la ubingwa wa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-23), baada ya kuibuka na ushindi katika mechi ya fainali ya michuano hiyo dhidi ya Burundi na kutwaa taji hilo. **PICHA: MTANDAO.**

# YANGA, BULLETS MAJARIBUNI LEO

### ●●● Ni katika mchezo wa ufunguzi wa michuano ya Kombe la Kagame ambayo...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA mara tano wa mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame, Yanga watawakaribisha Nyasa Big Bullets kutoka Malawi katika mechi ya ufunguzi ya michuano hiyo itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mechi hiyo itachezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam huku mabingwa mara sita, Simba wakijitoa kushiriki.

Akizungumza na gazeti hili jijini, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema wanatarajia kutambulisha wachezaji wao wapya ambao wanania ya kuwasajili kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki.

Bumbuli alisema wamejipanga kufanya vyema katika michuano hiyo na wanaamini watalinda heshima ya Tanzania ambao ndio wenyeji wa mashindano hayo.

Alisema wachezaji wao wapo tayari kupeperusha vyema bendera ya Yanga katika michuano hiyo iliyopangwa kumalizika ifikapo Agosti 15, mwaka huu.

"Tunawataka wanachama na mashabiki wa Yanga kuja kwa wingi kuisapoti timu yetu kwani tunataka kuchukua kombe hili kwa mara ya sita. Lakini haiwezekani lichezwe nchini halafu lichukuliwe na klabu nyingine kutoka nje," alisema Bumbuli na kuongeza.

"Kwenye michuano hii tutawatumia wachezaji ambao tunatarajia kuwasajili kwa ajili ya msimu ujao. Ina maana wachezaji wapya wa Yanga wataanza kuonekana kwenye michuano hii ya Kombe la Kagame. Na hata wale ambao hatujawaona, lakini tunataka kusajili, huu ndiyo wakati wao kutuonyesha vitu ambavyo vitafanya tuwasajili," Bumbuli alisema.

Yanga iliyopangwa Kundi A itashuka tena dimbani Agosti 4, mwaka huu kucheza dhidi ya Atlabala ya Sudan Kusini na itamaliza mechi zake za hatua ya makundi Jumamosi kwa kuwakabili Express kutoka Uganda.

Big Bullets ambayo zamani ilijulikana kwa jina la Bata Bullets, mara ya mwisho kucheza nchini Tanzania ilikuwa ni Novemba 16, mwaka 2018 dhidi ya Simba kwenye mechi ya kirafiki, na mchezo huo uliofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ulimalizika kwa sare ya bila kufungana.

Mechi ya utangulia inatarajiwa kuzikutanisha Express dhidi ya Atlabara na itachezwa kuanzia saa 10:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki.

Timu nane kutoka katika Ukanda wa CECAFA zitachuana ambapo Kundi A linaundwa na wenyeji Yanga, Nyasa Big Bullet, Atlabara na Express wakati KCCA (Uganda), Le Messager Ngozi kutoka Burundi, KMKM (Zanzibar) na Azam FC jijini ziko Kundi B ambalo litachezea mechi zake kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Mara ya mwisho michuano hiyo ilifanyika nchini Rwanda mwaka 2019 na KCCA ilifanikiwa kutwaa ubingwa baada ya kuichapa Azam FC bao 1-0 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamirambo.

9 770856 541002 >
GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042